# Mwongozo wa Wazazi wa Elimu Maalum

pamoja na Vidhibiti vya Kitaratibu



Kent ISD
We Lead Learning

## JEDWALI LA YALIYOMO

Wawasiliani wa Elimu Maalum kwenye Shule za Kienyeji ............... 1
Barua kwa Wazazi ........................................................................ 2
Mchakato wa Uelekezaji na Tathmini ............................................ 2
Miradi ya Elimu Iliyobinafsishwa (IEP) ........................................... 3
Ni yapi Mazingira Huria Zaidi (LRE)? ............................................. 3
Elimu ya Umma ya Bure iliyo Mwafaka (FAPE)? ............................ 3
Kushiriki kwa Wazazi na Wanafunzi kwenye IEP ........................... 3
Usafiri wa Elimu Maalum ............................................................... 3
Huduma na Miradi ya Elimu Maalum ............................................. 4
Orodha ya Rasilimali Zingine za Kuchapishwa Zinazopatikana ...... 4
Mashirika Yanayosaidia Wazazi .................................................... 5
Sera ya Kutobagua ........................................................................ 6
Vidhibiti vya Kitaratibu .................................................................... 7
Notisi ya Vidhibiti vya Kitaratibu ............................................... 7
Notisi ya Awali ya Kimaandishi ................................................ 7
Lugha ya Kiasili ....................................................................... 7
Barua Pepe ............................................................................. 7
Idhini ya Mzazi-Ufafanuzi ......................................................... 7
Idhini ya Mzazi ......................................................................... 7
Tathmini Huria za Elimu ........................................................... 9
Usiri wa Maelezo ...................................................................... 9
Ufafanuzi ............................................................................ 9
Maelezo Yanayotambulisha Kibinafsi ................................. 9
Notisi kwa Wazazi ............................................................... 9
Haki za Ufikiaji.................................................................... 10
Rekodi ya Ufikiaji ............................................................... 10
Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja ....................................... 10
Ada .................................................................................... 10
Kubadilisha Rekodi baada ya Ombi la Mzazi .................... 10
Fursa/Taratibu/Matokeo ya Kesi ....................................... 10
Idhini ya Ufichuzi ............................................................... 10
Vidhibiti/Uangamizi wa Maelezo/Haki za Mwanafunzi ....... 11
Upatanishi ..................................................................................... 11
Taratibu za Lalamishi kwa Jimbo .................................................. 11
Tofauti Baina ya Malalamishi na Kesi ............................... 11
Uidhinishaji wa Taratibu za Lalamishi kwa Jimbo .............. 11
Taratibu Zinazohitajika za Lalamishi kwa Jimbo ................ 12
Kuwasilisha Lalamishi kwa Jimbo ..................................... 12
Taratibu ya Lalamishi la Mchakato Yakinifu .................................. 12
Kuwasilisha Lalamishi la Mchakato Yakinifu ................................. 12
Lalamishi la Mchakato Yakinifu ....................................... 12
Fomu Teule ..................................................................... 13
Kusubiri Mtoto Kubadilishiwa Mandhari ya Elimu Wakati wa Lalamishi ......................................................................... 13
Mchakato wa Kusuluhisha ............................................... 13
Kesi kuhusu Malalamishi ya Mchakato Yakinifu ........................... 14
Kesi ya Mchakato Yakinifu Isiyobagua ............................. 14
Maamuzi/Haki kwenye Kesi ............................................. 14
Rufaa ............................................................................................ 14
Tamati ya Uamuzi; Rufaa; Tathmini Isiyobagua .............. 14
Muda na Uzingativu wa Kesi ........................................... 14
Hatua za Umma/Muda wa Kuwasilisha ............................ 15
Ada za Wakili ................................................................... 15
Taratibu za Kuwarekebisha Tabia Watoto wenye Ulemavu .......... 15
Hali Maalum - Mamlaka ya Waajiriwa Shuleni …………...16
Badiliko la Mandhari ya Elimu - Kuondolewa Shuleni kwa Tabia ................................................................................ 16
Uamuzi wa Mandhari ........................................................ 17
Rufaa ............................................................................... 17
Kubadilishiwa Mandhari ya Elimu Wakati wa Rufaa .......... 17
Ulinzi kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Husika......................................... 17
Uelekezaji hadi Watekelezaji Sheria na Mamlaka za Kimahakama na Hatua Zao..................... 17
Mahitaji ya Kubadilishiwa Mandhari ya Elimu Bila Kutushauri ambayo Inafanywa na Wazazi wa
Watoto kwenye Shule Binafsi kwa Gharama ya Umma........ 18
Uhamishi wa Haki za Wazazi anapofika Umri wa Utu Uzima . 18
Ufafanuzi wa Shirikisho........................................................ 18
Jeraha Kubwa Mwilini/Silaha ............................................18

## JINSI YA KUPATA HUDUMA

Ikiwa unadhani kuwa mtoto wako huenda anastahiki huduma za elimu maalum,ipigie simu wilaya yako ya shule. Mkurugenzi au msimamizi wa huduma na miradi ya elimu maalum kwenye wilaya yako ameorodheshwa hapo chini:

Shule za Umma za Kituo cha Byron, Erin Tacoma Simu: (616) 878-6121
Shule za Jamii za Caledonia, Alissa Hofstee Simu: (616) 891-0219
Shule za Umma za Cedar Springs, Stacey Jennette Simu: (616) 696-0580
Shule Huria
Mpigie simu Mwalimu Mkuu
Shule za Umma za Comstock Park, Jodi Miller Simu: (616) 254-5700
Shule za Umma za East Grand Rapids, Kathy Wisniewski Simu: (616) 235-3535
Shule za Umma za Forest Hills, Jann VanAirsdale Simu: (616) 493-8770
Shule za Umma za Godfrey Lee, Jane Dykhouse Simu: (616) 475-6622
Shule za Umma za Godwin Heights, David Baas Simu: (616) 252-2084
Shule za Umma za Grand Rapids, Teresita Long Simu: (616) 819-2185
Shule za Umma Grandville, Angie Thornburgh Simu: (616) 254-6768
Shule za Umma za Kelloggsville, Steve Brieve Simu: (616) 532-1585 au (616) 532-1590
Shule za Umma za Kenowa Hills, Dan Brant Simu: (616) 647-0910
Shule za Jamii za Mji wa Kent, Pam Thomas Simu: (616) 678-7714
Shule za Umma za Kentwood, Sharon O'Donnoghue Simu: (616) 554-3980
Shule za Eneo la Lowell, Mari Price Simu: (616) 987-2516
Shule za Umma za Northview, Dan Heitzman Simu: (616) 361-3446
Shule za Umma za Rockford, Kirsten Myers Simu: (616) 863-6326
Shule za Eneo la Sparta, Teresa Boyer Simu: (616) 887-7359
Shule za Thornapple Kellogg, Mari Price Simu: (269) 795-5571
Shule za Umma za Wyoming, Harry Knol Simu: (616) 530-7525

Orodha ya wasimamizi wa elimu maalum inayojumuisha anwani na nambari za faksi inapatikana kwenye Kent ISD.

# MWONGOZO WA WAZAZI WA ELIMU MAALUM

## Pamoja na Vidhibiti vya Kitaratibu

Ndugu Wazazi:

Tunakualika ujifahamishe kuhusu miradi, watu, na mashirika yanayopatikana ili kukusaidia wewe na mtoto wako.

Mwongozo huu unalenga wazazi wa watoto wenye ulemavu. Mwongozo huu ni chanzo kimoja cha maelezo kuhusu sheria za jimbo na shirikisho zilizoandikwa ili kulinda haki za wanafunzi wa elimu maalum. Nakala za ziada zitapatikana baada ya kupokea ombi kutoka kwa wilaya yako ya shule ya kienyeji au Kent ISD.

Washauri wa Wazazi wa Elimu Maalum (PASE) wanakukaribisha uhudhurie mikutano yetu. Ratiba inapatikana kutoka kwa Ofisi ya Elimu Maalum ya Kent ISD (365-2297).

Ikiwa ungependa maelezo ya ziada baada ya kupitia mwongozo huu, tafadhali wasiliana na wilaya yako ya shule ya kienyeji, Wilaya ya Shule ya Kimpito ya Kent, au ipigie simu Kent ISD ili kupata jina la mwakilishi wako wa PASE.

Kwa dhati,

**Laurie VanderPloeg**

Mkurugenzi wa Elimu Maalum wa Kent ISD

**Michael Ghareeb**

Naibu Mkurugenzi wa Elimu Maalum wa Kent ISD

**Rebecca McIntyre**

Msimamizi wa Elimu Maalum wa Kent ISD

**Amy Wooden**

Mwenyekiti wa Kent ISD PASE

---

### JE, ELIMU MAALUM NI NINI?

Elimu Maalum ni mafunzo yaliyotayarishwa kimahususi, bila gharama yoyote kwa mzazi, ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya mtoto mwenye ulemavu.

### JE, KWA NINI MTOTO WANGU ANAHITAJI KUFANYIWA TATHMINI?

Tathmini inafanywa ili kujibu maswali haya:

- Je, mtoto ana ulemavu?
- Je, matokeo ya mtoto yako vipi shuleni? (Kiwango cha hivi sasa cha matokeo kwenye masomo na utekelezaji wa shughuli)
- Je, mahitaji ya elimu ya mtoto ni yapi?
- Je, mtoto anahitaji elimu maalum na huduma husika?
- Je, maongezo au marekebisho yapi, yakiwepo, yanahitajika ili kumwezesha mtoto atimize shabaha za kila mwaka kwenye Mradi wa Elimu Uliobinafsishwa (IEP) na ashiriki, kama ni mwafaka, kwenye mtaala wa jumla?

### JE, NI ZIPI HATUA KWENYE TARATIBU YA TATHMINI?

Kabla ya mtoto kutathminiwa kwa mara ya kwanza, ni lazima shule imuarifu mzazi na ifafanue tathmini yoyote inayopendekezwa na shule kabla haijafanywa. Ni lazima mzazi atoe idhini yenye ufahamu ili mtoto aweze kutathminiwa.

Hatua ijayo inahusisha Timu ya IEP kukusanya na kuhakiki maelezo yaliyopo kuhusu mtoto. Hii inajumuisha kuzingatia maelezo, mazingatio, na tathmini za hivi sasa za darasani zinazotolewa na wazazi na waajiriwa shuleni.

### JE, MTOTO ANATATHMINIWA VIPI ILI KUNG'AMUA KUWEPO KWA ULEMAVU?

Mitihani inafanywa mmoja baada ya mwingine kwa lugha ya kiasili ya mtoto. Ni lazima mitihani iliyofanywa rasmi itumiwe kisahihi na kwa usawa na isimamiwe na wafanyakazi wenye elimu na waliofunzwa ili kuyafanya hayo.

### JE, NANI ANAAMUA KAMA MTOTO ANASTAHIKI HUDUMA?

Baada ya tathmini kukamilishwa, Timu ya IEP, inayojumuisha wataalamu wenye vyeti na mzazi, itaamua kama mtoto anastahiki elimu maalum.

### JE, NI YUPI "MTOTO MWENYE ULEMAVU?"

Ufafanuzi unajumuisha wanaokidhi yafuatayo:

- Watoto kuanzia wazaliwe mpaka wafike umri wa miaka 25 ambao hawajahitimu kwa kupokea diploma ya shule ya upili.
- Watoto wenye sifa za ulemavu maalum kama walivyofafanuliwa kwenye Sheria za Michigan za Elimu Maalum. (Tazama kategoria za elimu maalum zilizoorodheshwa kwenye kurasa za 4-5 za mwongozo huu.)
- Watoto ambao, kwa sababu ya ulemavu huo, wanahitaji elimu maalum na usaidizi wa huduma husika.

### JE, NINI KINATOKEA BAADA YA MTOTO/MWANAFUNZI KUPATIKANA KUWA ANASTAHIKI?

Kazi nyingine ya Timu ya IEP ni kuunda mradi wa mwanafunzi au Mradi wa Elimu Uliobinafsishwa (IEP). Kama ilivyobainishwa hapo awali, Timu ya IEP inajumuisha wazazi, wataalamu wa shule, na mwanafunzi, pale inapokuwa mwafaka. Baada ya IEP kuundwa, mwanafunzi anaanza kupokea elimu maalum na huduma husika kulingana na yale yanayokubaliwa na Timu ya IEP.

## JE, IEP NI NINI?

“Mradi wa Elimu Uliobinafsishwa” unamaanisha mpango wa kimaandishi wa mwanafunzi mwenye ulemavu unaobainisha elimu maalum na huduma husika zitakazopokewa na mwanafunzi. IEP inatayarishwa kwenye mkutano unaoratibiwa ufanyike kwenye wakati unaokubaliwa na wote. Hati ya kimaandishi ni rekodi ya mkutano wa Timu ya IEP. IEP inahakikiwa angalau mara moja kwa mwaka.

## JE, NINI KINAJUMUISHWA KWENYE IEP?

Mahitaji yanajumuisha:

- kauli ya kiwango cha hivi sasa cha matokeo kwenye masomo na utekelezaji wa shughuli
- kauli ya malengo ya muda mfupi na shabaha za kila mwaka zinazopimika ambazo zinashughulikia:
  1) jinsi ya kumsaidia mwanafunzi ajihusishe na astawi kwenye mtaala wa jumla, na
  2) jinsi ya kukidhi kila moja kati ya mahitaji mengine ya elimu ya mwanafunzi ambayo yanahusu ulemavu wake;
- kauli ya jinsi mwendeleo wa mwanafunzi unaelekea kufikia shabaha za kila mwaka utapimwa na jinsi wazazi watakavyokuwa wanafahamishwa kuhusu mwendeleo huo;
- kauli ya huduma/miradi ya elimu maalum na visaidizi vya ziada atakavyopewa mwanafunzi, na usaidizi au marekebisho yoyote ya mradi kwa wafanyakazi wa shule;
- kadirio la tarehe ya kuanza huduma na pia muda, marudio yanayotarajiwa, na eneo ambapo miradi na huduma zitafikishwa;
- ufafanuzi wa nyakati ambapo mwanafunzi hatoshiriki pamoja na watoto wasiokuwa walemavu kwenye madarasa ya kawaida na shughuli zingine;
- kauli kuhusu mabadiliko yoyote ambayo mwanafunzi atahitaji yafanywe ili aweze kufanya mitihani ya tathmini ya wilaya na/au jimbo; (Ikiwa Timu ya IEP inaamua kuwa mitihani hiyo si mwafaka kwa mwanafunzi, mbinu tofauti ya tathmini itatumiwa.)
- kauli ya huduma za mpito kuanzia umri wa miaka 16. Huduma za mpito zinajumuisha vipengele vingine vya maisha ya utu uzima na mara nyingine zinajumuisha mawakala mengine.

## JE, NI YAPI MAZINGIRA HURIA ZAIDI (LRE)?

LRE inatazama mazingira ambapo mwanafunzi anapokea elimu. Sheria inachukulia kuwa wanafunzi wenye walemavu wanapokea elimu vizuri zaidi wanapokuwa pamoja na wenzao wasiokuwa walemavu kwenye mandhari ya jumla ya elimu. Kuhudhuria darasa maalum au shule tofauti, au kuondoa wanafunzi wenye ulemavu kutoka kwenye darasa la kawaida kunatokea tu wakati asili au uzito wa ulemavu unamzuia asifanye vizuri kwenye masomo hata wakati huduma na visaidizi vya ziada vinatumika.

## JE, “ELIMU YA UMMA YA BURE ILIYO MWAFAKA” (FAPE) NI NINI?

FAPE inamaanisha elimu na huduma husika zinazotolewa kwa gharama ya umma, chini ya usimamizi na uelekezi wa umma, na bila gharama yoyote. Ni lazima huduma zinazotolewa zikidhi viwango vya Idara ya Elimu kwa wanafunzi wote na ziundwe ili kukidhi malengo ya muda mfupi na shabaha za IEP za mwanafunzi.

## JE, MZAZI ANASHIRIKI VIPI KWENYE TARATIBU YA KUFANYA UAMUZI?

Wazazi wanahimizwa wajihusishe kwa njia anuwai:

- Wazazi ni wanachama muhimu kwenye mikutano ya kufanya uamuzi kama vile mikutano inayoamua utambulisho, tathmini, daraja ya elimu, tathmini mpya, na elimu mwafaka ya mwanafunzi.
- Wazazi wanatoa idhini ya tathmini mpya na tathmini za awali.
- Wazazi watapokea ripoti za mara kwa mara kuhusu mwendeleo wa mwanafunzi wao.
- Ni lazima wazazi waiarifu wilaya ya shule iwapo wana nia ya kumuondoa mwanafunzi wao kutoka kwenye shule ya umma au ikiwa wanapanga

  kuwasilisha ombi la kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu.
- Wazazi wanahimizwa wajihusishe kwenye vikundi vya wazazi kwenye daraja ya kienyeji au kwenye daraja ya ISD kupitia kikundi cha ushauri kinachojulikana kama Washauri wa Wazazi wa Elimu Maalum (PASE). Idara ya Elimu ya Michigan pia inawahusisha wazazi kwenye kupanga, kutekeleza na kuhakiki shughuli.

## JE, MWANAFUNZI ANAFAA KUHUSISHWA KWENYE IEP?

Wanafunzi mara nyingi wanadhihirisha mawazo muhimu sana kuhusu nguvu na mahitaji yao. Wanapohusishwa kwenye uamuzi wa shabaha na malengo yao wenyewe, huwa wanajitolea zaidi kuyatimiza. Kila mwanafunzi anafaa kuwa na hiari ya kuwa kwenye taratibu ya Timu ya IEP.

Wanafunzi pia wanafaa kushiriki kwenye mipango yao wenyewe ya kimpito kabla hawajafika umri wa miaka 14, au wanapokuwa wadogo zaidi iwapo ni mwafaka. Mipango hii inasasishwa kila mwaka.

Mwanafunzi anapofika umri wa miaka 17, mwanafunzi na mzazi wanaarifiwa kuwa haki za mwanafunzi zitahamishwa hadi kwa mwanafunzi anapotimiza umri wa utu uzima (18). Anapofika umri wa miaka 18, mwanafunzi na wazazi wataarifiwa kuwa haki zao zimehamishwa.

## JE, WILAYA INAWAPATIA HUDUMA GANI YA USAFIRI WANAFUNZI WA ELIMU MAALUM?

Huduma sawia za usafiri zinazopatikana kwa wanafunzi wa elimu ya jumla pia zinapatikana kwa wanafunzi wa elimu maalum. Kwa ziada, huduma zilizobinafsishwa za usafiri zinatolewa na wilaya za shule iwapo Timu ya IEP inaamua kuwa mwanafunzi anahitaji huduma hizo ili kupokea elimu ya umma ya bure na iliyo mwafaka (FAPE). Majukumu ya wilaya ya shule yanayohusu usafiri yanajumuisha kuwapatia wanafunzi usafiri salama wenye ufanisi, kuweka tayari huduma zozote zilizobinafsishwa zilizorekodiwa kwenye IEP ya mwanafunzi (kama vile basi ya lifti au kamba za usalama za mabegani), na kufuata sheria na taratibu mwafaka za usalama, matibabu, na trafiki.

## JE, NI YAPI MAJUKUMU YANGU KUHUSU USAFIRI WA MTOTO WANGU MWENYE MAHITAJI MAALUM?

Ni muhimu wazazi/walezi wasome sera na taratibu za usalama zinazotolewa na ofisi yao ya wilaya au usafiri na kuzizungumzia sera hizo na

mtoto wako, iwapo itawezekana. Mbali na kuimarisha sheria za usalama, ni jukumu la wazazi kumsaidia mtoto wao apande basi ikiwa hawezi kusafiri peke yake baina ya makao yake na basi kwa ajili ya matatizo ya mwili, kutostawi vizuri, au kutofikika kwa makao. Mwanafunzi anaporudi kutoka shuleni, ni lazima mtu anayewajibika awe yuko nyumbani isipokuwa ikiwa mzazi/mlezi ametoa ruhusa ya kimaandishi ya kumuacha peke yake mwanafunzi mwenye umri mkubwa. Kufanya kazi pamoja, mawasiliano, na ushirikiano baina ya wazazi na shule ni muhimu ili kutimiza usafiri salama wa wanafunzi.

## JE, VIDHIBITI VYA KITARATIBU NI VIPI?

Ni vidhibiti vya kisheria vinavyolinda haki za wanafunzi wenye ulemavu na wazazi wao. Vinatoa maelezo yanayohitajiwa na wazazi ili kufanya uamuzi kuhusu elimu ya mtoto wao. Vinafafanua taratibu zinazotumiwa ili kutatua simtofahamu baina ya wahusika.

Vidhibiti vya Kitaratibu ndani ya kitabu hiki vinatoka kwenye sheria na kanuni za jimbo na shirikisho. Mara nyingine ni vigumu kuvielewa vidhibiti hivi. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu vidhibiti hivi, tafadhali wasiliana na Kent ISD, wilaya yako ya kienyeji ya shule, au vyanzo vilivyoorodheshwa kwenye jalada la mbele la mwongozo huu.

## HUDUMA NA MIRADI YA ELIMU MAALUM

Ni lazima kila wilaya ya shule ya kienyeji ifikishe au itolee kandarasi miradi na/au huduma maalum za elimu kwa wanafunzi wanaotambuliwa kuwa wana:

**Kasoro Mseto ya Otizimu** (ASD) – Watoto wenye mfululizo wenye kikomo wa vivutio na kasoro za uhodari wa kijamii na mawasiliano.
**Kasoro ya Akili** (CI) – Watoto waliokawia kwenye ustawi wao wa akili.
**Kiziwi-Kipofu** (DB) – Watoto wenye kasoro za kusikia na kuona; zote mbili kwa pamoja.
**Kukawia Kustawi Utotoni** (ECDD) – Watoto ambao, mpaka wanapofika umri wa miaka mitano, walikawia kustawi wenye kasoro isiyoweza kutambuliwa na kategoria yoyote nyingine.
**Kasoro ya Hisia** (EI) – Watoto wenye tabia na/au matatizo ya hisia yanayoathiri masomo.
**Kasoro ya Kusikia** (HI) – Watoto viziwi au wenye matatizo ya kusikia.
**Ulemavu wa Mafunzo** (LD) – Watoto wenye kasoro kwenye Mchakato wa mafunzo.
**Kasoro Nyingine ya Afya** (OHI) – Watoto wenye kasoro zingine za afya zinazoathiri mafunzo.
**Kasoro ya Mwili** (PI) – Watoto wenye kasoro za mwili zinazoathiri mafunzo.
**Kasoro Kadhaa Kubwa** (SXI) – Watoto wenye kasoro akilini na mwilini; zote mbili kwa pamoja.
**Kasoro ya Matamshi na Lugha** (SLI) – Watoto ambao hawajastawisha uhodari mwafaka wa matamshi, lugha, au mawasiliano.
**Jeraha Madhubuti la Ubongo** (TBI) – Watoto wenye jeraha la kichwa linaloathiri mafunzo yao.
**Kasoro ya Kuona** (VI ) – Watoto vipofu au wenye matatizo yakuona.

Timu ya Mradi wa Elimu Uliobinafsishwa (IEP), ambapo wewe ni mwanachama, inaamua miradi na/au huduma ambazo ni mwafaka kwa kila mwanafunzi. Timu ya IEP pia inaamua muda unaotumiwa kwenye elimu ya kawaida na elimu maalum.

Mwendelezo wa mandhari mbadala za elimu unapatikana kupitia shule huria au wilaya yako ya shule ya kienyeji. Mifano ya aina za miradi/huduma zinazopatikana inajumuisha huduma za Mwalimu Mshauri, Vyumba vya Rasilimali, madarasa yaliyobinafsishwa, na huduma anuwai husika.

Ikiwa Timu ya IEP inaamua kuwa mojawapo au zaidi kati ya huduma husika zinahitajika kwa mwanafunzi wako, kila wilaya ya shule ya kimpito, wilaya ya shule ya kienyeji, au shule huria ni lazima ifikishe au itolee kandarasi yafuatayo:

- Huduma za Audiolojia
- Tiba ya Kuzoeza Viungo
- Huduma za Utangulizi na Mwendo
- Tiba ya Kujishughulisha
- Huduma za Kisaikolojia
- Huduma za Kuhudumia Jamii za Shule
- Matamshi/Lugha/Mawasiliano
- Usafiri wa Tiba
- Huduma zingine husika kama inavyoamuliwa na Timu ya IEP

## ORODHA YA RASILIMALI ZINGINE ZINAZOPATIKANA KWENYE

**TOVUTI YETU HAPO: [www.kentisd.org](http://www.kentisd.org)**

- Mpango wa Elimu Maalum wa Kent ISD, unaojumuisha chati ambayo inafafanua aina ya miradi na huduma zinazopatikana kwenye ISD
- Orodha ya wasimamizi wa kienyeji wa elimu maalum inayojumuisha anwani, nambari za simu, na nambari za faksi
- Miongozo ya Ustahiki na Tathmini ya Kasoro Mseto ya Otizimu ya Kent ISD
- Miongozo ya Kuamua Ustahiki wa Kasoro ya Hisia ya Kent ISD
- Miongozo ya Tathmini ya Ulemavu wa Mafunzo ya Kent ISD
- Miongozo ya Tiba ya Kuzoeza Viungo ya Kent ISD
- Miongozo ya Tiba ya Kujishughulisha ya Kent ISD
- Miongozo ya Huduma, Ustahiki na Tathmini ya Lugha na Matamshi ya Kent ISD
- Maelezo yanayohusu kupata tathmini huria ya elimu
- Taratibu za Malalamishi za Elimu Maalum zilizoandikwa na Idara ya Elimu ya Michigan
- Orodha bainifu zaidi ya mashirika ya kienyeji na jimbo yanayosaidia wanafunzi wenye ulemavu na wazazi wao
- Maelezo kuhusu *Early On* ya Kaunti ya Kent, ushirikiano baina ya mawakala kadhaa ili kuwahudumia watoto kuanzia wanapozaliwa hadi wanapofika umri wa miaka mitatu.

**MASHIRIKA YANAYOSAIDIA WAZAZI**

**Mchakato wa Elimu Maalum: Kaunti ya Kent ya ARC**

Simu: (616) 459-3339, (800) 552-4821

www.arckent.org

**Idara ya Elimu ya Michigan**

Simu: (517) 373-0923

www.michigan.gov/mde

**Ulinzi na Utetezi wa Michigan**

Simu: (800) 288-5923

www.mpas.org

**Washauri wa Wazazi wa Elimu Maalum (PASE) wa ISD**

Simu: (616) 365-2297

www.kentisd.org/Special_Education/pase/

**Huduma Anazopewa Mtoto Wako: Chama cha Vipofu na wenye Kasoro za Kuona**

Simu: (616) 458-1187 au (800) 466-8084

www.abvimichigan.org

**Huduma za Ushauri za Arbor Circle**

Simu: (616) 459-7215

www.arborcircle.org

**Usaidizi wa Otizimu wa Kaunti ya Kent (ASK)**

Simu: (616) 752-8577

www.autismsupportofkentcounty.org

**Chama cha Otizimu cha Michigan**

Simu: (800) 223-6722 au (517) 882-2800

www.autism-mi.org

**Watoto na Watu Wazima wenye AD/HD (CHADD)**

Simu: (616) 874-5662

www.chaddgr.org or www.chadd.org

**Huduma za Uangalizi Maalum wa Afya za Watoto**

**Chama cha Down Syndrome cha Michigan Magharibi**

Simu: (866) 665-7451 au (616) 956-3488

www.dsawm.org

***Early On* ya Kaunti ya Kent**

Simu: (616) 365-2310

www.kentisd.org/earlyon

**Easter Seals Michigan, Inc.**

Simu: (800) 757-3257 au (616) 942-2081

www.essmichigan.org

Simu: (616) 632-7066

www.michigan.gov/cshcs

**Kituo Jumuishi cha Tiba (CTC)**

Simu: (616) 559-1054

www.therapycenter.org

**Msingi wa Uvimbe wa Fibrosisi**

Simu: (616) 956-6850

www.cff.org

**D.A. Blodgett-St. John's**

Simu: (616) 451-2021

www.dablodgettstjohns.org

**Watetezi wa Walemavu wa Kaunti ya Kent**

Simu: (616) 949-1100

www.dakc.us

**Family Futures**

Simu: (616) 454-4673

www.familyfutures.net

**Taasisi ya Family Hope**

Simu: (616) 780-3839

www.familyhopefoundation.org

**Goodwill Industries of Greater Grand Rapids**

Simu: (616) 532-4200

www.goodwillgr.org

**Heart of West Michigan Untied Way**

Simu: (616) 459-6281

www.hwmuw.org

**Kituo cha Kihispani cha Michigan Magharibi**

Simu: (616) 742-0200

www.hispanic-center.org

**Idara ya Huduma za Kibanadamu ya Kaunti ya Kent**

Simu: (616) 248-1000

www.michigan.gov/dhs

**Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent**

Simu: (616) 632-7100

www.accesskent.com

**Huduma za Ushauri za Leonard Street**

Simu: (616) 954-1991

www.lifeguidanceservices.org

**Chama cha Ulemavu wa Mafunzo cha Michigan**

Simu: (888) 597-7809 au (517) 485-8160

www.ldaofmichigan.org

**Muungano wa Familia wa Michigan**

Simu: (800) 552-4821

www.michiganallianceforfamilies.org

**Chama cha Distrofi ya Misuli (MDA)**

Simu: (616) 459-4331

www.mda.org

**Kituo cha Ufikiaji cha Network 180**

Simu: (616) 235-6604

www.network180.org

**Nyurofaibromatosisi Michigan**

Simu: (616) 451-3699

www.nfsupport.org

**Paragon (Hope Network Michigan Magharibi)**

Simu: (616) 719-2861

www.hopenetwork.org

**Huduma za Jamii za Spectrum**

Simu: (616) 241-6258

www.spectrumhuman.org

**Vigezo**

Simu: (616) 774-0853

www.threshnet.org

**United Cerebral Palsy (UCP) ya Michigan**

Simu: (800) 828-2714

www.ucpmichigan.org

## NOTISI YA SERA YA KUTOBAGUA

Ni sera ya wilaya ya shule kuwa hakuna mtu atakayemtenga mwingine kwa misingi ya rangi, asili ya kitaifa, imani au kizazi, imani za kisiasa, jinsia, ulemavu, dini, umri, kimo, uzito, au hali ya ndoa, ili asiweze kushiriki kwenye, asiweze kukataliwa manufaa ya, na asiweze kufanyiwa ubaguzi kwenye shughuli au mradi wowote na kwenye ajira pia.

Maswali yoyote kuhusu Kipengee cha IX cha Marekebisho ya Elimu ya 1972, kinachopiga marufuku ubaguzi kwa msingi wa jinsia, Kipengee cha VI, kinachopiga marufuku ubaguzi kwa msingi wa asilia, rangi, au asili ya kitaifa, au Kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973, kinachopiga marufuku ubaguzi kwa msingi wa ulemavu, yanafaa kuelekezwa kwa mkurugenzi wa elimu maalum aliyeorodheshwa kwenye ukurasa wa 1 wa hati hii.

## VIDHIBITI VYA KITARATIBU VINAVYOPATIKANA KWA WAZAZI WA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU

Hati hii inawapatia wazazi wa wanafunzi wenye ulemavu (wenye umri kuanzia wanapozaliwa mpaka wafike umri wa miaka 25 kuanzia Septemba 1 ya mwaka wa shule wa sasa) pamoja na muhtasari wa haki zao za elimu kuhusiana na elimu maalum. Hati hii inajumuisha vidhibiti vyote vya kitaratibu vinavyopewa wazazi na wanafunzi wenye ulemavu kwenye Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEA) na kanuni za utekelezaji za IDEA.

**Mafupisho yafuatayo yanatumiwa kwenye hati hii:**

| | |
|---|---|
| ALJ | Hakimu wa Sheria za Usimamizi |
| BIP | Mpango wa Kurekebisha Tabia |
| FAPE | Elimu Mwafaka ya Umma iliyo Bure |
| FERPA | Sheria ya Faragha na Haki za Elimu za Familia |
| FBA | Tathmini ya Matendo ya Kitabia |
| IDEA | Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu |
| IEE | Tathmini Huria ya Elimu |
| IEP | Mradi wa Elimu Uliobinafsishwa |
| MDE | Idara ya Elimu ya Michigan |
| OSE | Ofisi ya Elimu Maalum |
| SOAHR | Ofisi ya Jimbo ya Sheria na Kesi za Usimamizi |

## Notisi ya Vidhibiti vya Kitaratibu

Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEA), sheria ya Jimbo inayohusu wanafunzi wenye ulemavu, inazilazimu shule ziwapatie wazazi wa mtoto mwenye ulemavu notisi inayojumuisha ufafanuzi kamili wa vidhibiti vya kitaratibu vinavyopatikana kwenye IDEA na kanuni za Idara ya Elimu ya Marekani. Ni lazima nakala ya notisi hii ipatiwe wazazi tu mara moja kwa mwaka wa shule, isipokuwa kuwa ni lazima nakala ipatiwe wazazi : (1) baada ya uelekezaji au ombi la tathmini la mzazi; (2) baada ya kupokea lalamishi la kwanza kwa Jimbo kwenye 34 CFR §§300.151 kupitia

300.153 na baada ya kupokea lalamishi la kwanza la mchakato yakinifu kwa mujibu wa §300.507 kwenye mwaka wa shule; (3) uamuzi unapofanywa wa kuchukua hatua ya kurekebisha tabia unaojumuisha kubadilisha mandhari ya elimu; na (4) baada ya ombi la mzazi. [34 CFR 300.504(a)]. Ni lazima notisi ya vidhibiti vya kitaratibu ijumuishe ufafanuzi kamili wa vidhibiti vyote vya kitaratibu vinavyopatikana kwenye §300.148 (wazazi kuwaweka watoto kwenye shule binafsi kwa gharama ya umma), §§300.151 hadi 300.153 (taratibu za malalamishi za Jimbo), §300.300 (idhini), §§300.502 hadi 300.503, §§300.505 hadi 300.518, na §§300.530 hadi 300.536 (vidhibiti vya kitaratibu kwenye Kisehemu E cha kanuni za Sehemu B), na §§300.610 hadi 300.625 (usiri wa matakwa ya maelezo kwenye Kisehemu F).

## Notisi ya Awali ya Kimaandishi

34 CFR §300.503 Wilaya yako ya shule (maneno “wilaya ya shule,” kama yanavyotumiwa kwenye notisi hii, yanajumuisha shule ya umma) ni lazima ikupatie notisi ya kimaandishi (ikupatie maelezo fulani kimaandishi), kila wakati: (1) Inapopendekeza kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini, au mandhari ya elimu ya mtoto wako, au ufikishaji wa elimu mwafaka ya umma iliyo bure (FAPE) kwa mtoto wako; au (2) Inapokataa kuanzisha au kubadilisha

utambulisho, tathmini, au mandhari ya elimu ya mtoto wako, au ufikishaji wa FAPE kwa mtoto wako. Ni lazima notisi ya kimaandishi: (1) Ifafanue

hatua ambayo wilaya yako ya shule inapendekeza au inakataa ichukuliwe; (2) Ieleze kwa nini wilaya yako ya shule inapendekeza au inakataa kuchukua hatua; (3) Ifafanue kila taratibu, mtihani, rekodi, au ripoti ya tathmini iliyotumiwa na wilaya yako ya shule ili kuamua kuipendekeza au kuikataa hatua; (4) Ijumuishe kauli kuwa una ulinzi kwa mujibu wa matakwa ya vidhibiti vya kitaratibu kwenye Sehemu B ya IDEA; (5) Ikuambie jinsi unavyoweza kupata ufafanuzi wa vidhibiti vya kitaratibu iwapo hatua ambayo wilaya yako ya shule inaipendekeza au kuikataa si uelekezaji awali kwa tathmini; (6) Ijumuishe rasilimali za kuwasiliana nazo ili kupata usaidizi wa kuelewa Sehemu B ya IDEA; (7) Ifafanue machaguo yoyote mengine yaliyozingatiwa na mradi wa elimu uliobinafsishwa (IEP) wa mtoto wako na sababu kwa nini machaguo hayo yalikataliwa; na (8) Itoe ufafanuzi wa sababu zingine kwa nini wilaya yako ya shule iliipendekeza au kuikataa hatua. Wakala ya umma inaweza kutumia IEP kama sehemu ya notisi ya awali ya kimaandishi maadamu hati ambayo/ambazo zinapokewa na mzazi zinakidhi mahitaji yote yaliyoko kwenye §300.503. Ni lazima notisi: (1) Iandikwe kwa lugha inayoeleweka na watu kwa jumla; na (2) Itolewe kwa lugha ya kiasili au mbinu nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa ikiwa haiwezekani kufanya hivyo. Ikiwa lugha yako ya kiasili au mbinu nyingine ya mawasiliano si lugha ya kimaandishi, ni lazima wilaya yako ya shule ihakikishe kuwa: (1) Unafasiriwa notisi kwa mdomo, kwa mbinu nyingine kwenye lugha yako ya kiasili, au kwa mbinu nyingine ya mawasiliano; (2) Unaelewa maudhui ya notisi; na (3) Kuna ithibati ya kimaandishi kuwa 1 na 2 zimekidhiwa.

## Lugha ya Kiasili

34 CFR §300.29 *Lugha ya Kiasili,* inapotumiwa na mtu anayejua Kiingereza kidogo, inamaanisha yafuatayo: (1) Lugha ambayo kwa kawaida inatumiwa na mtu huyo, au, iwapo ni mtoto, lugha ambayo kwa kawaida inatumiwa na wazazi wa mtoto; (2) Kwenye mawasiliano yote ya moja kwa moja na mtoto (ikiwemo kumtathmini mtoto), lugha ambayo kwa kawaida inatumiwa na mtoto kwenye mazingira ya nyumbani au shuleni. Kwa mtu kiziwi au kipofu, au kwa mtu asiyekuwa na lugha ya kimaandishi, mbinu ya mawasiliano ni ile inayotumiwa kwa kawaida (lugha ya ishara, Braille, au mawasiliano ya matamshi).

## Barua Pepe

34 CFR §300.505 Ikiwa wilaya yako ya shule inawapatia wazazi hiari ya kupokea hati kupitia barua pepe, unaweza kuchagua kupokea yafuatayo kupitia baruapepe: (1) Notisi ya awali ya kimaandishi; (2) Notisi ya vidhibiti vya kitaratibu; na (3) Notisi kuhusu lalamishi la mchakato yakinifu.

## Idhini ya Mzazi - Ufafanuzi

34 CFR §300.9 *Idhini* inamaanisha: (1) Umefahamishwa kikamilifu kwa lugha yako ya kiasili au mbinu nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, Braille, au mawasiliano ya matamshi) juu ya maelezo yote kuhusu hatua ambayo unaitolea idhini. (2) Unaelewa na kukubaliana kimaandishi na hatua hiyo, na idhini inafafanua hatua hiyo na inaorodhesha rekodi (ikiwa zipo) zitakazotolewa na atakazopewa rekodi hizo; na (3) Unaelewa kuwa idhini ni hiari kwa upande wako na unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote. Uondoaji wako wa idhini haubatili (hautengui) hatua iliyotokea baada ya wewe kutoa idhini yako na kabla ya wewe kuiondoa idhini hiyo.

## Idhini ya Mzazi

34 CFR §300.300 Idhini ya tathmini za awali. Wilaya yako ya shule haiwezi kutekeleza tathmini ya awali ya mtoto wako ili kuamua kama mtoto wako anastahiki, kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, kupokea elimu maalum na huduma husika bila kwanza kukupatia mapema notisi ya kimaandishi ya hatua inayopendekezwa na bila kupata idhini yako kama ilivyofafanuliwa kwenye kichwa cha **Idhini ya Mzazi - Ufafanuzi**. Ni lazima wilaya yako ya shule ifanye juhudi zenye mantiki ili kupata idhini ya tathmini ya awali ili kuamua kama mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu. Idhini yako ya tathmini ya awali **haimaanishi** kuwa pia umetoa idhini yako ili wilaya ya shule ianze kumpatia mtoto wako elimu maalum na huduma husika. Ikiwa mtoto wako ameandikishwa kwenye shule ya umma au ikiwa unataka kumuandikisha mtoto wako na umekataa kutoa idhini au umeshindwa kujibu ombi la kutoa idhini ya tathmini ya awali, wilaya yako ya shule inaweza, lakini si lazima, itake kutekeleza tathmini ya awali ya mtoto wako kwa kutumia lalamishi la mchakato yakinifu au upatanishi, mkutano wa kusuluhisha, na taratibu za kesi za mchakato yakinifu zisizobagua. Wilaya yako ya shule haitokiuka majukumu yake ya kumweka pahali, kumtambua, na kumtathmini mtoto wako ikiwa haitofuatilia tathmini ya mtoto wako kwenye hali hizi.

**Sheria maalum za tathmini za wanaolelewa na Jimbo.** Ikiwa mtoto analelewa na Jimbo na haishi na mzazi wake —Wilaya ya shule haitohitaji idhini ya tathmini ya awali ili kuamua kama mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa: (1) Licha ya juhudi zenye mantiki za kufanya hivyo, wilaya ya shule haikuweza kumpata mzazi wa mtoto; (2) Haki za wazazi zimesitishwa kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; **au** (3) Hakimu au wakala ya umma yenye jukumu la uangalizi wa jumla wa mtoto imempatia haki ya kufanya maamuzi ya elimu na haki ya kutoa idhini ya awali kwa mtu ambaye si mzazi. *Anayelelewa na Jimbo*, kama inavyotumiwa kwenye IDEA, inamaanisha mtoto ambaye, ni: (1) Mtoto wa kulelewa, isipokuwa ikiwa mlezi wa mtoto amepewa haki ya kufanya maamuzi ya elimu kwa niaba ya mtoto na hakimu anayesimamia kesi ya mtoto au wakala ya umma yenye jukumu la uangalizi wa jumla wa mtoto; (2) Mtoto ambaye anachukuliwa kuwa ni anayelelewa na Jimbo kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; (3) Mtoto anayechukuliwa kuwa ni anayelelewa na mahakama kwa mujibu wa sheria ya Jimbo**; au** (4) Mtoto anayelelewa na wakala ya umma ya ustawi wa watoto.

**Idhini ya mzazi ya huduma**. Ni lazima wilaya ya shule ipate idhini yenye ufahamu kabla ya kumpatia mtoto wako elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, na ni lazima ifanye juhudi zenye mantiki ili kupata idhini yenye ufahamu. Usipoitikia ombi la kutoa idhini yako ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini hii, huenda wilaya yako ya shule isitumie vidhibiti vya kitaratibu (yaani, upatanishi, lalamishi la mchakato yakinifu, mkutano wa kusuluhisha, au kesi ya mchakato yakinifu isiyobagua) ili kupata makubaliano au uamuzi kuwa elimu maalum na huduma husika (zinazopendekezwa na Timu ya IEP ya mtoto wako) zinaweza kupewa mtoto wako bila idhini yako. Ukikataa kutoa idhini yako ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au ikiwa huitikii ombi la kutoa idhini hiyo na wilaya ya shule haimpatii mtoto wako elimu maalum na huduma husika ambazo kwa ajili ya hayo ilitaka idhini yako, wilaya yako ya shule: (1) Haikiuki mahitaji ya kuifanya FAPE ipatikane kwa mtoto wako kwa ajili ya kushindwa kumpatia mtoto wako huduma hizo; na (2) Haihitajiki ili kuwa na mkutano wa IEP au kumuundia mtoto wako IEP ya elimu maalum na huduma husika ambazo idhini yako inawasilishiwa ombi.

**Kubatilisha idhini ya mzazi.** Ukiifahamisha wilaya ya shule kimaandishi kuwa unabatilisha (unanyima) idhini yako inayoruhusu wilaya yako ya shule impatie mtoto wako elimu maalum na huduma husika, wilaya yako ya shule: (1) huenda isiendelee kumpatia mtoto wako elimu maalum na huduma husika; (2) ni lazima ikupatie notisi ya mapema ya kimaandishi kwa muda mwafaka, inayowiana na §300.503 ya kanuni za IDEA, kuhusu pendekezo lao la kusitisha elimu maalum na huduma husika kulingana na kupokea unyimaji idhini wako wa kimaandishi; (3) huenda isitumie taratibu za mchakato yakinifu (yaani, upatanishi, mkutano wa kusuluhisha, au kesi ya mchakato yakinifu isiyobagua) ili kupata makubaliano au uamuzi kuwa huduma zinaweza kupatiwa mtoto wako; (4) haikiuki mahitaji ya kuifanya FAPE ipatikane kwa mtoto wako kwa ajili ya kushindwa kumpatia mtoto wako elimu maalum na huduma husika za ziada; (5) si lazima ifanye mkutano au imuundie IEP mtoto wako ili kufikisha elimu maalum na huduma husika za ziada; na (6) si lazima irekebishe rekodi za elimu za mtoto wako ili kuondoa maelezo yoyote yanayorejelea mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma husika kwa sababu ya kubatilisha idhini.

**Idhini ya mzazi ya ufikishaji awali wa huduma.** Ni lazima wilaya yako ya shule ipate idhini yako yenye ufahamu kabla ya kumtathmini upya mtoto wako, isipokuwa ikiwa wilaya yako ya shule inaweza kuonyesha kuwa: (1) Ilichukua hatua zenye mantiki ili kupata idhini yako ya kumtathmini upya mtoto wako; na (2) Hukujibu. Ukikataa kutoa idhini ya kumtathmini upya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza, lakini si lazima, kufuatilia kumtathmini upya mtoto wako kwa kutumia upatanishi, lalamishi la mchakato yakinifu, mkutano wa kusuluhisha, na taratibu za kesi ya mchakato yakinifu isiyobagua ili kujaribu kushinda nguvu kukataa kwako kumtathmini upya mtoto wako. Kama vile tathmini za awali, wilaya yako ya shule haikiuki majukumu yake kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA ikikataa kufuatilia tathmini mpya kwa njia hii.

**Idhini ya mzazi ya kutoa maelezo ya Medicaid**. Ikiwa yoyote kati ya huduma zilizoorodheshwa hapo chini zinajumuishwa kwenye IEP ya mwanafunzi huyu, na ikiwa yeye anastahiki Medicaid wakati wowote kwenye utekelezaji wa IEP, mzazi ana hiari ya kukataa kutoa ruhusa ya kutoza mradi wa jimbo wa Medicaid ili kupokea fedha za kusaidia kufikisha huduma hizi. Huduma zinazosaidiwa na Medicaid zinajumuisha:

- Huduma za Teknolojia zenye Usaidizi
- Huduma za Uuguzi
- Tiba ya Kuzoeza Viungo
- Utangulizi na Mwendo
- Uangalizi wa Mwili
- Tiba ya Kujishughulisha
- Huduma za Kisaikolojia
- Huduma za Kuhudumia Jamii
- Tiba ya Matamshi/Lugha
- Usimamizi wa Kesi
- Usafiri

Kuutoza mradi wa jimbo wa Medicaid kwa Huduma Zinazotegemea Shule anazopokea mwanafunzi HAKUATHIRI fadhila za bima za Medicaid zinazopokewa na familia, na HAIGHARIMU familia sasa, wala HAIGHARIMU familia kwenye siku za usoni.

Kuutoza mradi wa jimbo wa Medicaid kunailazimu wilaya ya shule itume maelezo yanayomhusu mwanafunzi hadi kwa jimbo. Maelezo yanayotolewa yanaweza kujumuisha tarehe ya kuzaliwa, ulemavu, jinsia, shule, tarehe za huduma, aina ya huduma, na ripoti za mwendeleo. Wilaya shule zimekuwa zikiipatia jimbo maelezo haya tangu 1993.

Wazazi wana haki ya kukataa kutoa idhini ya kuutoza mfumo wa jimbo wa Medicaid, na wana haki ya kubatilisha idhini hii wakati wowote. Idhini ikikataliwa, wilaya ya shule itatoa huduma kwenye IEP, lakini haitopokea ufadhili kutoka kwa mfumo wa jimbo wa Medicaid wa kusaidia kulipia gharama za huduma hizi.

**Hati za juhudi zenye mantiki za kupata idhini ya mzazi.** Ni lazima shule yako idumishe hati za juhudi zenye mantiki za kupata idhini ya mzazi ya tathmini za awali, ili kufikisha elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, kwa lengo la kutathmini upya na kuwatafuta pale wazazi wa wanaolelewa na Jimbo walipo ili kutekeleza tathmini za awali. Ni lazima hati zijumuishe rekodi ya juhudi za wilaya ya shule kwenye maeneo haya, kama vile: (1) Rekodi bainifu za simu zilizopigwa au zilizojaribu kupigwa na matokeo ya simu hizo; (2) Nakala za mawasiliano zinazotumwa kwa wazazi na majibu yoyote yanayopokewa; na (3) Rekodi bainifu za ziara zilizofanywa nyumbani kwa mzazi au pahali pake pa ajira na matokeo ya ziara hizo.

**Mahitaji mengine ya idhini.** Idhini yako haihitajiki kabla ya wilaya yako ya shule: (1) Kupitia data iliyopo kama sehemu ya kumtathmini na kumtathmini upya mtoto wako; au (2) Kumpatia mtoto wako mtihani au tathmini nyingine inayopewa watoto wote isipokuwa kama, kabla ya mtihani au tathmini, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi wote wa watoto wote. Wilaya yako ya shule haifai kutumia kukataa kwako kutoa idhini ya shughuli au huduma moja ili kukunyima wewe au kumnyima mtoto wako shughuli, manufaa, au huduma yoyote nyingine. Ikiwa umemuandikisha mtoto wako kwenye shule binafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa mtoto wako anasoma nyumbani, na hutoi idhini ya mtoto wako kutathminiwa au kutathminiwa upya, au ukishindwa kujibu ombi la kutoa idhini yako, wilaya ya shule haifai kutumia idhini iliyopokea ili kuzizidi nguvu taratibu (yaani, upatanishi, lalamishi la mchakato yakinifu, mkutano wa kusuluhisha, au kesi ya mchakato yakinifu usiobagua) na si lazima imchukulie mtoto wako kuwa anastahiki kupokea huduma sawia (huduma zinazopatikana kwa watoto wenye ulemavu walioingizwa kwenye shule binafsi na mzazi.

**Tathmini Huria za Elimu**

34 CFR §300.502 Kama ilivyofafanuliwa hapo chini, una haki ya kupata tathmini huria ya elimu (IEE) ya mtoto wako ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako iliyopewa na wilaya yako ya shule. Ukiwasilisha ombi la IEE, ni lazima wilaya ya shule ikupatie maelezo kuhusu

kule unakoweza kupata IEE na kuhusu vigezo vya wilaya ya shule vinavyohusisha IEE. IEE inamaanisha kuwa tathmini inatekelezwa na mtahini mwenye cheti

ambaye hakuajiriwa na wilaya ya shule yenye jukumu la kumuelimisha mtoto wako. *Gharama ya umma* inamaanisha kuwa wilaya ya shule aidha inalipia gharama yote ya tathmini au inahakikisha kuwa unapokea tathmini kivingine bila gharama kwako, kwa kuwiana na matakwa ya Sehemu B ya IDEA, yanayoruhusu kila jimbo litumie vyanzo vyovyote vya usaidizi vya kienyeji, kishirikisho, na kibinafsi ambavyo vinapatikana kwenye jimbo ili kukidhi mahitaji ya Sehemu B ya Sheria. Una haki ya kupata IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako iliyopatikana na wilaya yako ya shule, kwa kutegemea masharti yafuatayo: (1) Ukiwasilisha ombi la kimaandishi la IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma, ni lazima wilaya yako ya shule ijibu, kimaandishi, ombi hilo ndani ya siku saba za kalenda baada ya kulipokea ombi, kwa kuashiria nia ya wilaya ya: (a) kutoa IEE kwa gharama ya umma; au (b) kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu la kuomba kusikizwa kesi ili kuonyesha kuwa tathmini yake ya mtoto wako ni mwafaka. (2) Ikiwa wilaya yako ya shule inawasilisha ombi la kusikizwa kesi na uamuzi wa mwisho ni kuwa tathmini ya wilaya yako ya shule iliyofanyiwa mtoto wako ni mwafaka, bado una haki ya kupokea IEE, lakini si kwa gharama ya umma. (3) Ukiwasilisha ombi la IEE ya mtoto wako, huenda wilaya ya shule ikakuuliza kwa nini unapinga tathmini ya mtoto wako iliyopewa na wilaya yako ya shule. Hata hivyo huenda wilaya yako ya shule isikulazimu ujieleze na huenda isikawie mno kufikisha IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma au kuwasilisha ombi la kesi ya mchakato yakinifu ili kutetea tathmini ya wilaya ya shule iliyofanyiwa mtoto wako. (4) Ikiwa IEE unayopata haikidhi vigezo vya wilaya ya shule, wilaya ya shule inaweza kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu. Ikiwa uamuzi wa mwisho wa kesi ni kuwa tathmini haikukidhi vigezo vya wilaya ya shule, fidia ya umma ya gharama ya IEE yako huenda ikakataliwa. Unastahiki IEE moja tu ya mtoto wako kwa gharama ya umma kila mara wilaya yako ya shule inapotekeleza tathmini ya mtoto wako ambayo hukubaliani nayo. Ikiwa unapata IEE ya mtoto wako kwa gharama ya umma au unaishiriki na wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako uliyopata kwa gharama ya umma: (1) Ni lazima wilaya yako ya shule izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa yanakidhi vigezo vya wilaya ya shule vya IEE, kwenye uamuzi wowote unaofanywa kuhusiana na ufikishaji wa FAPE kwa mtoto

wako; na (2) Wewe au wilaya yako ya shule inaweza kuionyesha tathmini hiyo kama ushahidi kwenye kesi ya mchakato yakinifu kuhusu mtoto wako. Ikiwa hakimu wa sheria ya usimamizi (ALJ) anawasilisha ombi la IEE la mtoto wako kama sehemu ya kesi ya mchakato yakinifu, ni lazima gharama ya tathmini iwe kwa gharama ya umma. Ikiwa IEE ni kwa gharama ya umma, vigezo vinavyotumiwa kupata tathmini, vikiwemo eneo la tathmini na vyeti vya mtahini, ni lazima viwe sawia kama vigezo ambavyo wilaya ya shule inavitumia inapoanzisha tathmini (kwa kiwango ambacho vigezo hivyo vinawiana na haki yako ya kufanyiwa IEE). Isipokuwa kwa vigezo vilivyofafanuliwa hapo juu, wilaya ya shule huenda isiweke masharti au vikomo vya muda vinavyohusu kupata IEE kwa gharama ya umma.

**Usiri wa Maelezo**

**Ufafanuzi -** 34 CFR §300.611 Kama inavyotumiwa kwenye kichwa cha **Usiri wa Maelezo**: *Uangamizi* inamaanisha uangamizi halisi au uondoaji wa vitambuaji vya kibinafsi kutoka kwenye maelezo ili maelezo hayo yasiweze kutambulisha tena kibinafsi, wakala, taasisi au wilaya ya shule inayokusanya, kudumisha, au kutumia maelezo yanayotambulisha kibinafsi, au *Rekodi za elimu* inamaanisha aina ya rekodi inayojumuishwa kwenye ufafanuzi wa ‘‘rekodi za elimu’’ kwa mujibu wa 34 CFR Sehemu ya 99 (kanuni zinazotekeleza Sheria ya Faragha na Haki za Elimu za Familia ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA)). FERPA inafafanua “rekodi za elimu” kama rekodi zinazohusiana moja kwa moja na mwanafunzi na zinazodumishwa na wakala ya elimu au mhusika anayefanya shughuli kwa niaba ya wakala. *Wakala inayoshiriki* inamaanisha wakala yoyote ambayo kutoka kwake maelezo yanapatikana, kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

**Maelezo Yanayotambulisha Kibinafsi** - 34 CFR §300.32 *Yanayotambulisha kibinafsi* inamaanisha maelezo yenye: (a) Jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mwanafamilia mwingine; (b) Anwani ya mtoto wako; (c) Kitambuaji cha kibinafsi, kama vile nambari ya mwanafunzi au nambari ya usalama wa kijamii ya mtoto wako; au (d) Orodha ya sifa za kibinafsi au maelezo mengine yanayoweza kuifanya iwezekane kumtambua mtoto wako kwa yakini yenye mantiki.

**Notisi kwa Wazazi** - 34 CFR §300.612 Ni lazima Idara ya Elimu ya Michigan (MDE) iwapatie notisi wazazi kuwa MDE ina taratibu na sera ambazo zinatosheleza ili kuwafahamisha kikamilifu wazazi kuhusu usiri wa maelezo yanayotambulisha kibinafsi, ikiwemo: (1) Ufafanuzi wa kiwango ambacho notisi inapewa kwa lugha za kiasili za vikundi anuwai vya watu kwenye Jimbo; (2) Ufafanuzi wa watoto ambao kwa ajili yao maelezo yanayotambulisha kibinafsi yanadumishwa, aina ya maelezo yanayotafutwa, mbinu ambazo Jimbo linanuia kutumia ili kukusanya maelezo (ikiwemo vyanzo ambapo maelezo hayo yalikusanywa, na njia ambazo maelezo hayo yatatumiwa; (3) Muhtasari wa sera na taratibu ambazo mawakala yanayoshiriki ni lazima yafuate kuhusiana na hifadhi, ufichuzi kwa watu wengine, ubakishaji, na uangamizi wa maelezo yanayotambulisha kibinafsi; na (4) Ufafanuzi wa haki zote za wazazi na watoto kuhusiana na maelezo haya, zikiwemo haki kwa mujibu wa FERPA na kanuni zake za utekelezaji kwenye 34 CFR Sehemu ya 99. Kabla ya shughuli yoyote kuu ya utambulishaji, eneo, au tathmini (pia inajulikana kama “utafutaji mtoto”), ni lazima notisi ichapishwe au itangazwe kwenye magazeti au vyombo vingine, au zote mbili, isambae kwa kutosha ili kuwaarifu wazazi kwenye Jimbo zima kuhusu shughuli hiyo ili kuwatafuta, kuwatambua, na kuwatathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma husika.

**Haki za Ufikiaji** - 34 CFR §300.613 Ni lazima wakala inayoshiriki ikuruhusu ukague na upitie rekodi zinazohusu mtoto wako zinazokusanywa, kudumishwa, au kutumiwa na wakala inayoshiriki kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. Ni lazima wakala inayoshiriki itii ombi lako la kukagua na kupitia rekodi zozote za elimu kuhusu mtoto wako bila kukawia kusikoeleweka kabla ya mkutano wowote kuhusu IEP, au kesi yoyote ya mchakato yakinifu usiobagua (ikiwemo mkutano wa kusuluhisha au kesi kuhusu tabia), na hakuna hali ambapo itakuwa zaidi ya siku 45 za kalenda baada ya wewe kuwasilisha ombi. Haki yako ya kukagua na kupitia rekodi za elimu inajumuisha: (1) Haki yako ya kupokea jibu kutoka kwa wakala inayoshiriki uliyoitumia maombi yenye mantiki ya ufafanuzi na ufasiri wa rekodi; (2 )Haki yako ya kuwasilisha ombi kuwa wakala inayoshiriki itoe nakala za rekodi ikiwa huwezi kukagua na kuhakiki kwa ufanisi isipokuwa ikiwa utapokea nakala hizo; na (3) Haki yako ya mwakilishi wako kuzikagua na kuzihakiki rekodi. Wakala inayoshiriki inaweza kuchukulia kuwa una mamlaka ya kukagua na kuhakiki rekodi zinazohusu mtoto wako isipokuwa ikiwa unashauriwa kuwa huna mamlaka kwa mujibu wa sheria husika ya Jimbo inayotawala mambo kama vile ulezi, au utengano na talaka.

**Rekodi ya Ufikiaji -** 34 CFR §300.614 Ni lazima kila wakala inayoshiriki idumishe rekodi ya wahusika wanaoweza kufikia rekodi za elimu zinazokusanywa, kudumishwa, au kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (isipokuwa ufikiaji unaofanywa na wazazi na waajiriwa walioidhinishwa na wakala inayoshiriki), ikiwamo jina la mhusika, tarehe ufikiaji ulipewa, na lengo ambalo kwa ajili yake mhusika ameruhusiwa kuzitumia rekodi.

**Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja -** 34 CFR §300.615 Ikiwa rekodi yoyote ya elimu inajumuisha maelezo kuhusu zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kuyakagua na kuyahakiki tu maelezo yanayohusu mtoto wao au kufahamishwa kuhusu maelezo hayo maalum.

**Orodha ya Aina na Maeneo ya Maelezo -** 34 CFR §300.616 Baada ya kupokea ombi, ni lazima kila wakala inayoshiriki ikupatie orodha ya aina na maeneo ya rekodi za elimu zilizokusanywa, kudumishwa au kutumiwa na wakala.

**Ada -** 34 CFR §300.617 Kila wakala inayoshiriki inaweza kutoza ada ya nakala za rekodi unazofanyiwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwa ada hiyo haikuzuii usiweze kutekeleza haki yako ya kuzikagua na kuzihakiki rekodi hizo. Wakala inayoshiriki haifai kutoza ada ya kutafuta au kupokea maelezo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

**Kubadilisha Rekodi baada ya Ombi la Mzazi -** 34 CFR §300.618 Ikiwa unaamini kuwa maelezo kwenye rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kudumishwa, au kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA si sahihi, yanapotosha, au yanakiuka haki zingine za mtoto wako, unaweza kuwasilisha ombi kwa wakala inayoshiriki inayoyadumisha maelezo ili kuyabadilisha maelezo hayo. Ni lazima wakala inayoshiriki iamue kama itabadilisha maelezo kulingana na ombi lako ndani ya kipindi mwafaka cha muda baada ya kupokea ombi lako. Ikiwa wakala inayoshiriki itakataa kubadilisha maelezo kulingana na ombi lako, ni lazima ikufahamishe kuwa imekataa na ikushauri kuhusu haki ya kusikizwa kesi kama ilivyofafanuliwa kwenye kichwa, **Fursa ya Kusikizwa Kesi**.

**Fursa ya Kusikizwa Kesi -** 34 CFR §300.619 Ni lazima wakala inayoshiriki, baada ya kupokea ombi, ikupatie fursa ya kusikizwa kesi ya kuyapinga maelezo yaliyoko kwenye rekodi za elimu yanayomhusu mtoto wako ili kuhakikisha kuwa ni sahihi, hayapotoshi, wala kivingine hayakiuki faragha au haki zingine za mtoto wako.

**Taratibu za Kusikizwa Kesi -** 34 CFR §300.621 Ni lazima kesi ya kupinga maelezo yaliyoko kwenye rekodi za elimu itekelezwe kulingana na taratibu za kesi hizi kwa mujibu wa FERPA.

**Matokeo ya Kesi -** 34 CFR §300.620 ikiwa, kutokana na kusikizwa kesi, wilaya inayoshiriki inaamua kuwa maelezo si sahihi, yanapotosha au kivingine yanakiuka faragha au haki zingine za mtoto, ni lazima iyabadilishe maelezo vilivyo na ikufahamishe kimaandishi. Ikiwa, kutokana na kesi hiyo, wilaya inayoshiriki inaamua kuwa maelezo hayo si sahihi, yanapotosha au kivingine yanakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako, ni lazima ikufahamishe kuhusu haki yako ya kuweka kwenye rekodi zinazodumishwa, kauli ya mtoto wako inayotoa maelezo au inayotoa sababu zozote kwa nini hukubaliani na uamuzi wa wakala inayoshiriki. Ni lazima ufafanuzi huo unaowekwa kwenye rekodi za mtoto wako: (1) Udumishwe na wilaya inayoshiriki kama sehemu ya rekodi za mtoto wako maadamu rekodi au sehemu yenye utetezi inadumishwa na wakala inayoshiriki; na (2) Ikiwa wakala inayoshiriki itafichua rekodi za mtoto wako au sehemu yenye utetezi kwa mhusika mwingine, ni lazima pia ufafanuzi huo upewe mhusika huyo mwingine.

**Idhini ya Ufichuzi wa Maelezo Yanayotambulisha Kibinafsi -** 34 CFR §300.622 Isipokuwa ikiwa ufichuzi wa maelezo yanayotambulisha kibinafsi yaliyoko kwenye rekodi za elimu (bila idhini ya mzazi) unaidhinishwa kwa mujibu wa FERPA, ni lazima idhini yako ipatikane kabla maelezo yanayotambulisha kibinafsi kufichuliwa kwa wahusika wengine ambao si maafisa wa mawakala yanayoshiriki. Isipokuwa kwenye hali zilizobainishwa hapo chini, idhini yako haihitajiki kabla ya maelezo yanayotambulisha kibinafsi kupewa maafisa wa mawakala yanayoshiriki kwa malengo ya kukidhi mahitaji ya Sehemu B ya IDEA. Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefika umri wa utu uzima kwa mujibu wa sheria ya Jimbo, ni lazima ipatikane kabla ya maelezo yanayotambulisha kibinafsi kupewa maafisa wa mawakala yanayoshiriki yanayotoa au yanayolipia huduma za mpito. Ikiwa mtoto wako yuko kwenye, au ataingizwa kwenye, shule binafsi ambayo haiko kwenye wilaya sawia na shule ya pale unapoishi, ni lazima idhini yako ipatikane kabla maelezo yoyote yanayotambulisha kibinafsi kuhusu mtoto wako yapewe maafisa kwenye wilaya ya shule ambapo shule binafsi ipo na maafisa kwenye wilaya ya shule ambapo wewe unaishi.

**Vidhibiti** - 34 CFR §300.623 Ni lazima kila wakala inayoshiriki ilinde usiri wa maelezo yanayotambulisha kibinafsi kwenye hatua za kukusanywa, kuhifadhiwa, kufichuliwa, na kuharibika kwa maelezo hayo. Ni lazima afisa mmoja kwenye kila wakala inayoshiriki achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa maelezo yoyote yanayotambulisha kibinafsi. Ni lazima watu wote wanaokusanya au kutumia maelezo yanayotambulisha kibinafsi wapokee ukufunzi au mafunzo kuhusu sera na taratibu a Michigan kuhusiana na usiri kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na FERPA. Ni lazima kila wakala inayoshiriki idumishe, ili iweze kukaguliwa na umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya wale waajiriwa ambao huenda wanaweza kufikia maelezo yanayotambulisha kibinafsi.

**Uangamizi wa Maelezo** - 34 CFR §300.624 Ni lazima wilaya yako ya shule ikufahamishe wakati maelezo yanayotambulisha kibinafsi yanakusanywa, kudumishwa au kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA yanapokuwa hayahitajiki tena ili kumpatia mtoto wako huduma za elimu. Ni lazima

maelezo yaangamizwe baada ya kupokea ombi lako. Hata hivyo, rekodi ya milele ya jina, anwani, na nambari ya simu ya mtoto wako, matokeo yake ya mitihani, rekodi ya kufika shuleni, darasa alizohudhuria, daraja ya darasa aliyotimiza, na mwaka wa kumaliza yanaweza kudumishwa bila kikomo cha muda.

**Haki za Mwanafunzi -** 34 CFR §300.625 Kwa mujibu wa kanuni za FERPA, haki za wazazi kuhusiana na rekodi za elimu zinahamishwa hadi kwa mwanafunzi anapofika umri wa miaka 18. Haki za wazazi kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kuhusiana na rekodi za elimu pia zinahamishwa hadi kwa mwanafunzi anapofika umri wa miaka 18. Hata hivyo, ni lazima wakala inayoshiriki itoe notisi yoyote inayohitajika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kwa mwanafunzi na wazazi.

## Upatanishi

34 CFR §300.506 MDE imeunda taratibu za kuufanya upatanishi upatikane kwa kukuruhusu wewe na kuiruhusu shule itatue simtofahamu kuhusu jambo lolote kwa mujibu wa Sehemu B au Sehemu C ya IDEA, ikiwemo mambo yanayoibuka kabla ya kuwasilisha lalamishi la jimbo au lalamishi la mchakato yakinifu. Kwa hivyo, upatanishi unapatikana ili kusuluhisha simtofahamu kwa mujibu wa Sehemu B au Sehemu C ya IDEA, kama umewasilisha lalamishi la mchakato yakinifu au la ili kuwasilisha ombi la kesi ya mchakato yakinifu kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Kuwasilisha Lalamishi la Mchakato Yakinifu.** Taratibu zinahakikisha kuwa mchakato wa upatanishi: (1) Ni hiari kwa upande wako na kwa upande wa wilaya ya shule; (2) Hautumiwi ili kunyima au kukawisha haki yako ya kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu, au kuzikataa haki zozote zingine ulizo nazo kwa mujibu wa Sehemu B au Sehemu C ya IDEA; na (3) Unatekelezwa na mpatanishi asiyebagua na mwenye vyeti aliyefunzwa mbinu zenye ufanisi za upatanishi. Wilaya ya shule inaweza kuunda taratibu zinazowapatia wazazi na shule zinazochagua kutotumia mchakato wa upatanishi, fursa ya kukutana, kwenye wakati na eneo unalopendelea, na mhusika asiyekuwa na maslahi kwenye mambo haya: (1) Ambaye amefanya mkataba na shirika mbadala lililo mwafaka la kusuluhisha simtofahamu, au kituo cha maelezo na mafunzo kwa wazazi au kituo cha jamii cha rasilimali za wazazi kwenye Jimbo; na (2) Ambaye angeeleza manufaa na kukuhimizia matumizi ya mchakato wa upatanishi. Ni lazima MDE idumishe orodha ya watu ambao ni wapatanishi wenye vyeti na wanaojua sheria na kanuni zinazohusu ufikishaji wa elimu maalum na huduma husika. Ni lazima MDE ichague wapatanishi bila mpangilio, kwa mzunguko au bila kubagua. Jimbo lina jukumu la kugharimia mchakato wa upatanishi, ikiwemo gharama za mikutano. Huduma hizi zinatolewa na Mradi wa Upatanishi wa Elimu Maalum wa Michigan hapo http://www.cenmi.org/msemp. Ni lazima kila mkutano kwenye mchakato wa upatanishi uratibiwe kwa muda mwafaka na ufanywe kwenye sehemu unayopendelea na sehemu inayopendelewa na wilaya ya shule. Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtasuluhisha simtofahamu kupitia mchakato wa upatanishi, ni lazima wahusika wote wawili wafanye makubaliano yanayowafunganisha kisheria yanayobainisha suluhisho na: (1) Yanayobainisha kuwa mahojiano yote yaliyotokea wakati wa mchakato wa upatanishi yatabakia kuwa ya siri na hayafai kutumiwa kama ushahidi kwenye taratibu yoyote ya mahakama ya umma au kesi yoyote ya mchakato yakinifu itakayokuja mbeleni; and (2) Yanatiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule mwenye mamlaka ya kuifunganisha kisheria wilaya ya shule. Makubaliano ya kimaandishi yaliyotiwa saini yanatekelezeka kisheria kwenye mahakama yoyote ya Jimbo kwenye mamlaka adilifu (mahakama yenye mamlaka ya kusikiza kesi kama hii kwa mujibu wa sheria ya Jimbo) au kwenye mahakama ya wilaya nchini Marekani. Ni lazima mahojiano yaliyofanyika wakati wa mchakato wa upatanishi yabakie kuwa ya siri. Hayawezi kutumiwa kama ushahidi kwenye taratibu yoyote ya mahakama ya umma au kesi yoyote ya mchakato yakinifu itakayokuja mbele ya mahakama yoyote ya jimbo au shirikisho ya jimbo linalopokea msaada kwa mujibu wa Sehemu B na Sehemu C ya IDEA.

**Mpatanishi kutobagua -** Mpatanishi: (1) Hafai kuwa mwajiriwa wa MDE au wilaya ya shule inayohusishwa kwenye elimu au uangalizi wa mtoto wako; na (2) Hafai kuwa na maslahi ya kikazi au kibinafsi yanayoenda kinyume na kuangalia usawa kwa mpatanishi. Mtu ambaye kivingine anastahiki kuwa mpatanishi si mwajiriwa wa wilaya ya shule au wakala ya Jimbo tu kwa sababu yeye analipwa na wakala au wilaya ya shule ili afanye kazi kama mpatanishi.

## Taratibu za Lalamishi kwa Jimbo

**Tofauti Baina ya Lalamishi la Kesi ya Mchakato Yakinifu na Taratibu za Lalamishi kwa Jimbo -** Kanuni za Sehemu B ya IDEA zilizobainishwa kwenye taratibu tofauti za malalamishi kwa Jimbo na kwa kesi na malalamishi ya mchakato yakinifu. Kama ilivyofafanuliwa hapo chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha lalamishi la

Jimbo linalodai ukiukaji wa masharti yoyote kwenye Sehemu B au Sehemu C uliofanywa na wilaya ya shule, MDE, au wakala yoyote nyingine ya umma. Wewe au wilaya ya shule tu

inaweza kuwasilisha lalamishi kwa mchakato yakinifu kuhusu jambo lolote kuhusu pendekezo au katazo la kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au ubadilishaji mandhari ya elimu kwa mtoto mwenye ulemavu, au ufikishaji wa FAPE kwa mtoto. Ingawa kwa jumla ni lazima waajiriwa wa MDE wasuluhishe lalamishi la Jimbo ndani ya muda wa siku 60 za kalenda, isipokuwa ikiwa muda huo unaongezwa kupitia mbinu mwafaka, ni lazima ALJ isikize kesi ya lalamishi la mchakato yakinifu (ikiwa halikusuluhishwa kupitia mkutano wa kusuluhisha au kupitia upatanishi) na iwakilishe uamuzi wa kimaandishi ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha, kama inavyofafanuliwa kwenye hati hii kwa mujibu wa kichwa, **Mchakato wa Kusuluhisha**, isipokuwa ikiwa ALJ inaruhusu upanuzi maalum wa muda baada ya wewe kuwasilisha ombi au baada ya wilaya

ya shule kuwasilisha ombi. Lalamishi kwa Jimbo na lalamishi la mchakato yakinifu, taratibu za kesi na usuluhishaji zinaelezwa kikamilifu zaidi hapo chini.

**Uidhinishaji wa Taratibu za Lalamishi kwa Jimbo -** 34 CFR §300.151 Ni lazima MDE iwe na taratibu za kimaandishi (tazama Sheria za Usimamizi za Elimu Maalum, Sheria ya 340.1701a, 340.1851-1853) ya: (1) Kusuluhisha lalamishi lolote kwa Jimbo, ikiwemo lalamishi lililowasilishwa na shirika au mtu binafsi anayetoka kwenye Jimbo lingine; (2) Kuwasilisha lalamishi; (3) Kusambaza kwa upana taratibu za lalamishi kwa Jimbo hadi kwa wazazi na watu wengine wenye maslahi, ikiwemo vituo vya maelezo na mafunzo kwa wazazi, mawakala ya ulinzi na utetezi, vituo huria vya kuishi, na mashirika mengine husika. Kwenye usuluhishaji wa lalamishi kwa Jimbo ambapo MDE imeng'amua kushindwa kufikisha huduma mwafaka, ni lazima MDE ishughulikie: (1) Kushindwa kufikisha huduma mwafaka, ikiwemo hatua za urekebishaji zilizo mwafaka ili kuyashughulikia mahitaji ya mtoto; na (2) Ufikishaji mwafaka wa huduma kwenye siku za usoni kwa watoto wote wenye ulemavu.

**Taratibu Zinazohitajika za Lalamishi kwa Jimbo -** 34 CFR §300.152 MDE, kupitia Ofisi ya Elimu Maalum (OSE), itajumuisha kwenye taratibu zake za lalamishi kwa Jimbo, kikomo cha muda wa siku 60 za kalenda baada ya lalamishi kuwasilishwa kwa: (1) Kutekeleza uchunguzi huria kituoni, ikiwa MDE inaamua kuwa uchunguzi unahitajika; (2) Kumpatia mlalamishi fursa ya kuwasilisha maelezo ya ziada, iwe ni kimatamshi au kimaandishi, kuhusu madai kwenye lalamishi; (3) Kuipatia wilaya ya shule au wakala ya umma fursa ya kulijibu lalamishi, ikiwemo, kwa kiwango cha chini kabisa: (a) kwa hiari ya wakala, pendekezo la kusuluhisha lalamishi; na (b) fursa kwa mzazi aliyewasilisha lalamishi na wakala kukubali kwa hiari kujihusisha kwenye upatanishi; (4) Kuhakiki maelezo yote husika na kufanya uamuzi huria kama wilaya ya shule inakiuka sharti la Sehemu B ya IDEA au la; na (5) Kumpatia mlalamishi uamuzi wa kimaandishi unaoshughulikia kila dai kwenye lalamishi na unaojumuisha: (a) matokeo ya ukweli na makataa; na (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa MDE. Taratibu za MDE zilizofafanuliwa hapo juu pia ni lazima: (1) Ziruhusu upanuzi wa kikomo cha muda wa siku 60 za kalenda tu ikiwa: (a) hali za kipekee zipo kuhusiana na lalamishi fulani la Jimbo; au (b) mzazi na wilaya ya shule au wakala nyingine ya umma inayohusishwa ikubali kwa hiari kuupanua muda wa kulisuluhisha jambo kupitia upatanishi; (2) Zijumuishe taratibu za utekelezaji wenye ufanisi wa uamuzi wa mwisho wa MDE, ikiwa inabidi, ikiwemo: (a) shughuli za usaidizi wa kiufundi; (b) mazungumzo; na (c) hatua za urekebishaji ili kutimiza utiifu. Ikiwa lalamishi la kimaandishi la Jimbo linapokewa ambalo pia limehusishwa kwenye kesi ya mchakato yakinifu kama ilivyofafanuliwa hapo chini kwa mujibu wa kichwa, **Kuwasilisha Lalamishi la Mchakato Yakinifu**, au lalamishi la Jimbo linajumuisha masuala kadhaa ambayo moja au zaidi ni sehemu ya kesi hii, ni lazima Jimbo liweke kando lalamishi la Jimbo, au sehemu yoyote ya lalamishi la Jimbo ambalo linashughulikiwa kwenye kesi ya mchakato yakinifu mpaka kesi hiyo ikamilike. Tatizo lolote kwenye lalamishi la Jimbo ambalo si sehemu ya kesi ya mchakato yakinifu ni lazima lisuluhishwe kwa kutumia taratibu na kikomo cha muda kilichofafanuliwa hapo juu. Ikiwa tatizo linaloibuka kwenye lalamishi kwa Jimbo tayari limetolewa uamuzi kwenye kesi ya mchakato yakinifu inayoshusisha wahusika sawia (wewe na wilaya ya shule), basi kesi ya mchakato yakinifu inafunganisha kisheria kuhusiana na suala hili na ni lazima MDE imfahamishe mlalamishi kuwa uamuzi unafunganisha kisheria. Lalamishi linalodai kuwa wilaya ya shule au wakala ya umma imeshindwa kutekeleza kesi ya mchakato yakinifu ni lazima lisuluhishwe na MDE.

**Kuwasilisha Lalamishi kwa Jimbo -** 34 CFR §300.153 Shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha lalamishi kwa Jimbo lililotiwa saini kwa mujibu wa taratibu zilizofafanuliwa hapo juu. Lalamishi kwa Jimbo ni lazima lijumuishe: (1) Kauli kuwa wilaya ya shule au wakala nyingine ya umma imekiuka: (a) Matakwa yoyote ya sasa ya sheria za usimamizi za elimu maalum; (b) 1976 PA 451, MCL 380.1 et seq., kuhusiana na miradi na huduma za elimu maalum; (c) Sheria ya elimu ya watu wenye ulemavu ya 2004, 20 U.S.C., sura ya 33, §1400 et seq., na kanuni zinazotekeleza sheria hiyo, 34 C.F.R. Sehemu ya 300, na 34 C.F.R. sehemu ya 303; (d) Mpango wa wilaya ya shule wa kimpito; (e) Ripoti ya timu ya mradi wa elimu uliobinafsishwa, uamuzi wa afisa wa kesi, uamuzi wa mahakama kuhusiana na miradi na huduma za elimu maalum; au (f)Ombi kwa jimbo ili kupokea fedha za shirikisho kwa mujibu wa IDEA; (2) Maelezo halisi ambayo kauli hiyo inategemea; (3) Saini na maelezo ya mawasiliano ya mlalamishi, na (4) Ikiwa inadai ukiukaji kuhusu mtoto maalum: (a) Jina la mtoto na anwani ya makaazi ya mtoto; (b) Jina la shule ambayo mtoto anahudhuria; (c) Iwapo mtoto au kijana hana makao, maelezo ya mawasiliano yanayopatikana ya mtoto huyo, na jina la shule ambayo mtoto huyo anahudhuria; (d) Ufafanuzi wa asili ya tatizo la mtoto huyo, ikiwemo maelezo halisi kuhusu tatizo hilo; na (e) Suluhisho linalopendekezewa tatizo hilo kwa kiwango ambacho linajulikana na linapatikana kwa mhusika anayewasilisha lalamishi wakati lalamishi linapowasilishwa. Ni lazima lalamishi lidai ukiukaji uliotokea si zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo lalamishi linapokewa na MDE au ISD. Ni lazima mhusika anayewasilisha lalamishi kwa Jimbo asambaze nakala ya lalamishi kwa wilaya ya shule au wakala nyingine ya umma inayomhudumia mtoto wakati huo huo ambapo mhusika anawasilisha lalamishi kwa OSE. MDE imeunda fomu teule ili kusaidia kuwasilisha lalamishi kwa Jimbo. Fomu teule inapatikana hapo www.michigan.gov/ose-eis. Si lazima utumie fomu teule. Hata hivyo, ni lazima lalamishi lijumuishe maelezo yanayohitajika ili kuwasilisha lalamishi kwa Jimbo (Tazama 1-4 hapo juu).

## Taratibu za Lalamishi la Mchakato Yakinifu

**Kuwasilisha Lalamishi la Mchakato Yakinifu -** 34 CFR §300.507 Wewe au wilaya ya shule inaweza kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu juu ya jambo lolote kuhusu pendekezo au katazo la kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au ubadilishaji mandhari ya elimu ya mtoto wako, au ufikishaji wa FAPE kwa mtoto wako. Ni lazima lalamishi la mchakato yakinifu lidai kuwa ukiukaji ambao ulitokea si zaidi ya miaka miwili kabla ya wakati ambapo wewe au wilaya ya shule ilijua au ilikuwa inafaa

kujua kuhusu tendo linalodaiwa ambalo linaunda msingi wa lalamishi la mchakato yakinifu. Mfuatilio wa muda wa hapo juu haukuhusishi ikiwa hukuweza kuwasilisha

lalamishi la mchakato yakinifu ndani ya muda mwafaka kwa sababu: (1) Wilaya ya shule imedanganya kimahususi kuwa ilikuwa imesuluhisha matatizo yaliyokuwa yametambuliwa kwenye lalamishi; au (2) Wilaya ya shule haikukupatia maelezo ambayo ilikuwa ni lazima ikupatie kwa mujibu wa Sehemu B au Sehemu C ya IDEA. Ni lazima wilaya ya shule ikufahamishe kuhusu huduma za bure au zinazogharimu kidogo za kisheria na huduma zingine husika zinazopatikana kwenye eneo hilo ikiwa utayaulizia maelezo hayo, au ikiwa wewe au wilaya ya shule itawasilisha lalamishi la mchakato yakinifu.

**Lalamishi la Mchakato Yakinifu -** 34 CFR §300.508 Ili kuwasilisha ombi la kesi, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) ni lazima iwasilishe lalamishi la mchakato yakinifu kwa MDE, na impatie nakala mhusika mwingine. Ni lazima lalamishi lijumuishe maudhui yote yaliyoorodheshwa hapo chini na ni lazima usiri wake udumishwe. Ni lazima lalamishi la mchakato yakinifu lijumuishe: (1) Jina la mtoto; (2) Anwani ya makaazi ya mtoto;

(3) Jina la shule ya mtoto; (4) Ikiwa mtoto ni mtoto au kijana asiyekuwa na makao, maelezo ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto; (5)Ufafanuzi wa asili ya tatizo la mtoto kuhusiana na hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa, ikiwemo maelezo halisi kuhusu tatizo hilo; na (6) Suluhisho linalopendekezwa la tatizo hilo kwa kiwango ambacho linajulikana na linapatikana kwako au kwa wilaya ya shule kwenye wakati huo. Wewe au wilaya ya shule haifai kuwa na kesi ya mchakato yakinifu mpaka wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule), awasilishe kwa njia mwafaka lalamishi la mchakato yakinifu linalojumuisha maelezo ya hapo juu. Lalamishi la mchakato yakinifu linachukuliwa kuwa limewasilishwa kwa njia mwafaka wakati linapokuwa limepokewa na MDE na mhusika mwingine. Ili lalamishi la mchakato yakinifu liendelee mbele, ni lazima lichukuliwe kuwa linatosheleza mahitaji yote. Lalamishi la mchakato yakinifu litazingatiwa kuwa linatosheleza mahitaji yote (limekidhi mahitaji yote ya maudhui yaliyotajwa hapo juu) isipokuwa ikiwa mhusika anayepokea lalamishi la mchakato yakinifu (wewe au wilaya ya shule) aiarifu ALJ na mhusika mwingine kimaandishi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea lalamishi, kuwa mhusika anayepokea anaamini kuwa lalamishi la mchakato yakinifu halikidhi mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu. Ndani ya siku tano za kalenda baada ya kupokea taarifa, mhusika anayepokea (wewe au wilaya ya shule) anachukulia kuwa lalamishi la mchakato yakinifu halikidhi mahitaji yote, ni lazima ALJ iamue kama lalamishi la mchakato yakinifu linakidhi mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu, na ikuarifu wewe na wilaya ya shule kwa maandishi papo hapo. Wewe au wilaya ya shule mnaweza kufanya mabadiliko kwenye lalamishi hilo tu ikiwa: (1) Mhusika mwingine anaidhinisha mabadiliko kimaandishi na anapewa fursa ya kusuluhisha lalamishi la mchakato yakinifu kupitia mkutano wa kusuluhisha, uliofafanuliwa hapo chini; au (2) ALJ inatoa ruhusa mabadiliko hayo yafanywe, si zaidi ya siku tano kabla ya kesi ya mchakato yakinifu kuanza. Ikiwa mhusika anayelalamika (wewe au wilaya ya shule) anafanya mabadiliko kwenye lalamishi la mchakato yakinifu, muda wa kufanywa mkutano wa kusuluhisha (ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea lalamishi) na kipindi cha muda wa kusuluhisha (ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea lalamishi) kitaanzishwa tena kwenye tarehe ambapo lalamishi lililorekebishwa linawasilishwa. Ikiwa wilaya ya shule haijakutumia notisi ya awali, kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Notisi ya Awali ya Kimaandishi**, kuhusiana na maudhui yaliyojumuishwa kwenye lalamishi lako la mchakato yakinifu, ni lazima wilaya ya shule, ndani ya siku 10 za kalenda, ikutumie jibu linalojumuisha: (1) Ufafanuzi wa kwa nini wilaya ya shule ilipendekeza au ilikataa hatua iliyoibuka kwenye lalamishi la mchakato yakinifu; (2) Ufafanuzi wa machaguo mengine ambayo Timu ya IEP ya mtoto wako yaliyazingatia na kwa nini machaguo hayo yalikataliwa; (3) Ufafanuzi wa kila taratibu, tathmini, rekodi, au ripoti ya ukaguzi iliyotumiwa na shule kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa; na (4) Ufafanuzi wa sababu zingine ambazo zinahusu hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa ya wilaya ya shule. Kufikisha maelezo kwenye vipengee vya 1-4 hapo juu hakuizui wilaya ya shule isibainishe kuwa lalamishi lako la mchakato yakinifu lilikuwa halitoshelezi mahitaji. Isipokuwa kama imebainishwa kwa mujibu wa kichwa kidogo kilichoko hapo juu karibu kwenye hati hii, **Jibu la lalamishi la mchakato yakinifu la wilaya ya shule**, ni lazima mhusika anayepokea lalamishi la mchakato yakinifu, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea lalamishi, amtumie mhusika mwingine jibu linalobainisha kimahususi masuala yaliyoko kwenye lalamishi.

**Fomu Teule -** 34 CFR §300.509 MDE imeunda fomu teule ili kukusaidia kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu. Si lazima utumie fomu teule ya MDE. Hata hivyo, ni lazima lalamishi la mchakato yakinifu lipate maelezo yote yanayohitajika ili kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu. Fomu teule inapatikana hapo www.michigan.gov/ose-eis. (Dokezo: Matumizi ya fomu teule hayahakikishi kuwa ALJ ingeona kuwa lalamishi halitoshelezi mahitaji yote ikiwa mhusika mwingine anapinga kutosheleza mahitaji kwa lalamishi hilo.)

**Mandhari ya Elimu ya Mtoto Wakati Kesi na Lalamishi la Mchakato Yakinifu Zinasubiriwa -** 34 CFR §300.518 Isipokuwa kama ilivyobainishwa hapo chini kwa mujibu wa kichwa**, Taratibu za Kuwarekebisha Tabia Watoto wenye Ulemavu,** pindi lalamishi la mchakato yakinifu linapowasilishwa na MDE na kupokewa na mhusika mwingine, ni lazima mtoto wako abakie kwenye shule yake ya sasa wakati wa kipindi cha muda cha mchakato wa kusuluhisha, isipokuwa ikiwa wewe na Jimbo au wilaya ya shule mnakubaliana kivingine. Ikiwa lalamishi la mchakato yakinifu linahusisha ombi kukubaliwa awali kwenye shule ya umma, mtoto wako, baada ya kupokea idhini yako, ni lazima aingizwe kwenye mradi wa kawaida wa shule ya umma mpaka taratibu zote hizi zikamilike. Ikiwa lalamishi la mchakato yakinifu linahusisha ombi la kupokea huduma za awali kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA ya mtoto ambaye hali yake inabadilika kutoka kuhudumiwa kwa mujibu wa Sehemu C ya IDEA hadi Sehemu B ya IDEA na ambaye hastahiki tena huduma za Sehemu C kwa sababu mtoto amefika umri wa miaka mitatu, si lazima wilaya ya shule iendelee kufikisha huduma za Sehemu C ambazo mtoto alikuwa anazipokea. Ikiwa mtoto anapatikana kuwa anastahiki kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na unatoa idhini ili mtoto wako apokee

elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, basi, kwa kusubiri mwendeleo wa kesi, ni lazima wilaya ya shule ifikishe elimu maalum na huduma husika ambazo hazina simtofahamu (zile ambazo wewe na wilaya ya shule mmekubaliana nazo).

**Mchakato wa Kusuluhisha -** 34 CFR §300.510 Ni lazima wilaya ya shule ifanye mkutano wa kusuluhisha unaojumuisha wewe na mwanachama au wanachama husika wa Timu ya IEP ambao wana elimu maalum kuhusu maelezo halisi yaliyotambuliwa kwenye lalamishi lako la mchakato yakinifu. Ni lazima mkutano wa kusuluhisha ufanywe ndani ya siku 15 za kalenda baada ya lalamishi la mchakato yakinifu kuwasilishwa kwa MDE, na kupokewa na wilaya ya shule. Kesi ya mchakato yakinifu haiwezi kuanza mpaka mkutano wa kusuluhisha ufanyike. Mkutano: (1) Ni lazima ujumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; na (2) Haufai kujumuisha wakili wa wilaya ya shule isipokuwa ikiwa unaandamana na wakili. Wewe na wilaya ya shule mnaamua wanachama husika wa Timu ya IEP watakaohudhuria mkutano. Lengo la mkutano ni wewe uweze kuzungumzia lalamishi lako la mchakato yakinifu, na maelezo halisi yanayounda msingi wa lalamishi hilo, ili wilaya ya shule iwe na fursa ya kuisuluhisha simtofahamu. Mkutano wa kusuluhisha hauhitajiki ikiwa: (1) Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kimaandishi kutofanya mkutano; au (2) Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kutumia mchakato wa upatanishi, kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Upatanishi**. Ikiwa wilaya ya shule haijasuluhisha lalamishi la mchakato yakinifu mpaka ukaridhika ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea lalamishi la mchakato yakinifu (wakati wa kipindi cha muda cha mchakato yakinifu), kesi ya mchakato yakinifu inaweza kusikizwa. Muda wa siku 45 za kalenda wa kufanya uamuzi unaanza baada ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, isipokuwa kukiwa na vitengwa maalum vya marekebisho yanayofanywa kwenye kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, kama ilivyofafanuliwa hapo chini. Isipokuwa pale wewe na wilaya ya shule nyote mmekubaliana kutokuwa na mchakato wa kusuluhisha au kutotumia upatanishi, kushindwa kwako kushiriki kwenye mkutano wa kusuluhisha kutafanya mchakato wa kusuluhisha na kesi ya mchakato yakinifu zikawie mpaka ushiriki kwenye mkutano. Ikiwa baada ya kufanya juhudi zenye mantiki na kurekodi juhudi hizo, wilaya ya shule haikuweza kukufanya wewe ushiriki kwenye mkutano wa kusuluhisha, wilaya ya shule inaweza, baada ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, kuwasilisha ombi kuwa ALJ inafaa kupuuza lalamishi lako la mchakato yakinifu. Ni lazima rekodi za juhudi hizi zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule ya kupanga sehemu na wakati unaokubalika na pande zote wa kufanya mkutano huo, kama vile: (1) Rekodi bainifu za simu zilizopigwa au zilizojaribu kupigwa na matokeo ya simu hizo; (2) Nakala za mawasiliano ulizotumiwa na majibu yoyote yanayopokewa; na (3) Rekodi bainifu za ziara zilizofanywa nyumbani kwako au pahali pako pa ajira na matokeo ya ziara hizo. Wilaya ya shule ikishindwa kufanya mkutano wa kusuluhisha ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea notisi ya lalamishi lako la mchakato yakinifu, au ikishindwa kushiriki kwenye mkutano wa kusuluhisha, unaweza kuambia ALJ itoe agizo la kuanzisha muda wa kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu wa siku 45 za kalenda. Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kimaandishi kutofanya mkutano wa kusuluhisha, muda wa siku 45 za kalenda wa kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu utaanza siku ifuatayo. Baada ya kuanza kwa mkutano wa kusuluhisha au mkutano wa upatanishi na kabla ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30, ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kimaandishi kuwa hakuna makubaliano yanayoweza kupatikana, muda wa siku 45 za kalenda wa kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu utaanza siku ifuatayo. Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubali kutumia mchakato wa upatanishi, baada ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, wahusika wote wawili wanaweza kukubaliana kimaandishi kuwa waendelee na mchakato wa upatanishi mpaka wakubaliane. Hata hivyo, ikiwa wewe au wilaya ya shule baadaye mnajitoa kwenye mchakato wa upatanishi, muda wa siku 45 za kalenda wa kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu utaanza siku ifuatayo. Ikiwa suluhisho la simtofahamu linapatikana kwenye mkutano wa kusuluhisha, ni lazima wewe na wilaya ya shule mufanye makubaliano yanayowafunganisha kisheria ambayo: (1) Yanatiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule mwenye mamlaka ya kuifunganisha kisheria wilaya ya shule; na (2) Yanatekelezeka kisheria na mahakama ya jimbo lolote lenye mamlaka adilifu (mahakama ya jimbo yenye mamlaka ya kusikiza aina hii ya kesi) au kwenye mahakama ya wilaya nchini Marekani. Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnafanya makubaliano yanayotokana na mkutano wa kusuluhisha, mhusika yoyote (wewe au wilaya ya shule) mnaweza kughairi makubaliano ndani ya siku 3 rasmi baada ya wakati ambapo wewe na wilaya ya shule mliyatia saini makubaliano hayo.

**Kesi za Malalamishi ya Mchakato Yakinifu**

**Kesi ya Mchakato Yakinifu Isiyobagua -** 34 CFR §300.511 Wakati wowote lalamishi la mchakato yakinifu lisilobagua linapowasilishwa, ni lazima wewe au wilaya ya shule inayohusishwa kwenye simtofahamu ipewe fursa ya kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu isiyobagua, baada ya kufuata taratibu zilizofafanuliwa kwenye vifungu vya **Lalamishi la Mchakato Yakinifu** na **Mchakato wa Kusuluhisha**.

**Hakimu wa sheria ya usimamizi asiyebagua -** Kwa kiwango cha chini kabisa, ALJ: (1) Ni lazima awe si mwajiriwa wa MDE au wilaya ya shule inayohusishwa kwenye elimu au uangalizi wa mtoto huyo. Hata hivyo, mtu si mwajiriwa wa wakala tu kwa sababu yeye analipwa na wakala ili afanye kazi kama ALJ;

(2) Ni lazima asiwe na maslahi ya kibinafsi au kikazi yanayoenda kinyume na ufuataji haki wa ALJ wakati wa kusikiza kesi; (3) Ni lazima awe anayafahamu na anayaelewa matakwa ya IDEA, na kanuni za jimbo na shirikisho zinazohusu IDEA, na ufasiri wa kisheria wa IDEA unaofanywa na mahakama za shirikisho na jimbo, na (4) Ni lazima awe na ufahamu na uwezo wa kusikiza kesi, na kufanya na kuandika uamuzi, unaowiana na utendakazi wa kisheria ulio mwafaka na uliozoewa. ALJ ni waajiriwa wa huduma za umma waliojumuishwa na Jimbo ambao ni mawakili na ambao wameajiriwa na Ofisi ya Jimbo ya Sheria na Kesi za Usimamizi (SOAHR). MDE (kupitia SOAHR) inadumisha orodha inayojumuisha vyeti vya wale

wanaofanya kazi kama ALJ.

**Maudhui ya kesi ya mchakato yakinifu -** Mhusika (wewe au wilaya ya shule) ambaye anawasilisha ombi la mchakato yakinifu huenda asiibue maswala kwenye kesi ya mchakato yakinifu ambayo hayakushughulikiwa kwenye lalamishi la mchakato yakinifu, isipokuwa ikiwa mhusika mwingine anakubaliana na hayo.

**Muda wa kuwasilisha ombi la kusikizwa kesi -** Ni lazima wewe au wilaya ya shule muwasilishe lalamishi la mchakato yakinifu ndani ya miaka miwili baada ya tarehe ambapo wewe au wilaya ya shule ilijua au ilikuwa inafaa kujua kuhusu suala/masuala yanayoshughulikiwa kwenye lalamishi.

**Vitengwa vya muda -** Muda wa hapo juu haukuhusishi ikiwa hukuweza kuwasilisha lalamishi la mchakato yakinifu kwa sababu: (1) Wilaya ya shule imedanganya kimahususi kuwa ilikuwa imesuluhisha tatizo au suala unaloibua kwenye lalamishi lako; au (2) Wilaya ya shule haikupatia maelezo ambayo ilikuwa ni lazima yakupatie kwa mujibu wa Sehemu B au Sehemu C ya IDEA.

**Haki za Kesi -** 34 CFR §300.512 Mhusika wowote kwenye kesi ya mchakato yakinifu (ikiwemo kesi kuhusu taratibu za urekebishaji tabia) ana haki ya (1) Kuandamana na kushauriwa na wakili na/au watu wenye elimu au ufahamu kuhusu matatizo ya watu wenye ulemavu; (2) Kuonyesha ushahidi na kupinga, kuhoji, na kulazimu kuhudhuria kwa mashahidi; (3) Kukataza utangulizi wa ushahidi wowote kwenye kesi ambao haujafichuliwa kwa mhusika huyo angalau siku tano za kibiashara kabla ya kusikizwa kesi; (4) Kupata rekodi ya kimaandishi, au, kwa hiari yako, rekodi ya elektroniki ya neno kwa neno ya kusikizwa kesi; na (5) Kupata matokeo ya kimaandishi, au, kwa hiari yako, matokeo ya elektroniki ya ukweli na uamuzi. Angalau siku tano za kibiashara kabla ya kesi ya mchakato yakinifu, wewe au wilaya yako ya shule ni lazima ifichue kwa mwenzake tathmini zote zingine zilizokamilishwa kabla ya tarehe hiyo na mapendekezo yanayotokana na tathmini hizo ambayo wewe au wilaya ya shule inayanuia kutumia wakati wa kusikiza kesi. ALJ inaweza kumzuia mhusika yoyote anayeshindwa kutii mahitaji haya asitangulize tathmini au pendekezo husika kwenye kesi bila idhini ya mhusika mwingine. Ni lazima upewe haki ya: (1) Kuwepo kwa mtoto wako; (2) Kuisikiza kesi hadharani; na (3) Kupewa rekodi ya kusikizwa kesi, matokeo ya ukweli na uamuzi bila kutozwa chochote.

**Maamuzi ya Kesi - 34 CFR §300.513** Uamuzi wa ALJ wa kama mtoto wako amepokea FAPE ni lazima utegemee misingi madhubuti. Kwenye masuala yanayodai ukiukaji wa kitaratibu, ALJ inaweza kung'amua kuwa mtoto wako hakupokea FAPE tu ikiwa upungufu wa kitaratibu: (1) Ulienda kinyume na haki ya mtoto wako ya kupata FAPE; (2) Ulienda kinyume sana na fursa yako ya kushiriki kwenye mchakato wa kufanya uamuzi kuhusiana na kumfikishia FAPE mtoto wako; au (3) Ulisababisha upungufu wa manufaa ya elimu.

**Kipengee cha ujenzi -** Hakuna matakwa yaliyofafanuliwa hapo juu ambayo yatafasiriwa kuwa yanaizuia ALJ isiagize wilaya ya shule itii mahitaji kwenye kipengee cha vidhibiti vya kitaratibu cha kanuni za shirikisho kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536).

**Ombi tofauti la kesi ya mchakato yakinifu -** Hakuna chochote kwenye kifungu cha vidhibiti vya kitaratibu cha kanuni za shirikisho kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536) kinachoweza kufasiriwa kuwa kinakuzuia usiwasilishe lalamishi tofauti la mchakato yakinifu kuhusu tatizo lililo tofauti na lalamishi la mchakato yakinifu ambalo tayari limewasilishwa.

**Matokeo na uamuzi kwa jopo la ushauri na umma wote -** MDE, baada ya kufuta maelezo yote yanayotambulisha kibinafsi, ni lazima: (1) Iyafikishe matokeo na maamuzi kwenye kesi ya mchakato yakinifu hadi kwa kamati ya ushauri ya elimu maalum ya jimbo; na (2) Iyafanye matokeo na maamuzi hayo yapatikane kwa umma.

## Rufaa

**Tamati ya Uamuzi; Rufaa; Tathmini Isiyobagua -** 34 CFR §300.514 Uamuzi unaofanywa kwenye kesi ya mchakato yakinifu (ikiwemo kesi inayohusu taratibu za urekebishaji tabia) ni wa mwisho, isipokuwa kuwa mhusika yoyote anayehusishwa kwenye kesi (wewe au wilaya ya shule) anaweza kuukatia rufaa uamuzi kwa kuleta hatua ya

umma, kama inavyofafanuliwa hapo chini.

**Muda na Uzingativu wa Kesi -** 34 CFR §300.515 Ni lazima MDE ihakikishe kuwa si zaidi ya siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha siku 30 za kalenda cha mikutano ya kusuluhisha au, si baada ya siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha muda kilichorekebishwa kama kinavyofafanuliwa kwa mujibu wa

Kichwa kidogo, **Marekebisho kwenye kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda**: (1) Uamuzi wa mwisho unafanywa kwenye kesi; na (2) Nakala ya uamuzi inatumwa kwa barua kwa kila mhusika. ALJ inaweza kuruhusu upanuzi wa muda upite kipindi cha muda cha siku 45 za kalenda kama inavyofafanuliwa hapo juu baada ya kupokea ombi la mhusika yoyote baina ya hao wawili. Ni lazima kila kesi itekelezwe kwenye wakati na sehemu ambapo wewe na mtoto wako mnaipendelea.

**Hatua za Umma, Zikiwemo Kipindi cha Muda cha Kuwasilisha Hatua Hizo -** 34 CFR §300.516 Mhusika yoyote (wewe au wilaya ya shule) asiyekubaliana na matokeo na uamuzi kwenye kesi ya mchakato yakinifu (ikiwemo kesi inayohusu taratibu za urekebishaji tabia) ana haki ya kuleta hatua ya umma kuhusiana na jambo lililokuwa mada ya kesi ya mchakato yakinifu. Hatua inweza kuletwa kwenye mahakama ya jimbo kwenye mamlaka adilifu (mahakama ya jimbo yenye mamlaka ya kusikiza aina hii ya kesi) au kwenye mahakama ya wilaya nchini Marekani bila kujali thamani ya simtofahamu. Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayeleta hatua atakuwa na siku 90 za kalenda kuanzia tarehe ya uamuzi wa ALJ ili kuwasilisha hatua ya umma. Kwenye hatua yoyote ya umma, mahakama: (1) Inapokea rekodi za taratibu za usimamizi; (2) Inasikiza ushahidi wa ziada baada ya kupokea ombi lako au baada ya kupokea ombi la wilaya ya shule; na (3) Inafanya uamuzi wake kwa msingi wa ukaguzi wa ushahidi na inatoa fidia inayoamuliwa kuwa mwafaka na mahakama.

**Mamlaka ya mahakama za wilaya -** Mahakama za wilaya za Marekani zina mamlaka ya kufanya uamuzi wa hatua zinazoletwa mahakamani kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA bila kujali thamani ya simtofahamu.

**Sheria ya ujenzi -** Hakuna chochote kwenye Sehemu B ya IDEA kitakachozuia au kuwekea kikomo haki, taratibu, na tiba zinazopatikana kwa mujibu wa Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu ya 1990, Mada ya V ya Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973 (Kifungu cha 504), au sheria zingine za shirikisho zinazolinda haki za watoto wenye ulemavu, isipokuwa kuwa kabla ya kuwasilisha hatua ya umma kwa mujibu wa sheria hizi ili kupata fidia ambayo pia inapatikana kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, taratibu za mchakato yakinifu zilizofafanuliwa hapo juu ni lazima zidhoofishwe kwa kiwango sawia kama kile ambacho kingehitajika ikiwa mhusika aliwasilisha hatua kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. Hii inamaanisha kuwa kuna tiba zinazopatikana kwa mujibu wa sheria zingine zinazokinzana na zile zinazopatikana kwa mujibu wa IDEA, lakini kwa jumla, ili kupata fidia kwa mujibu wa sheria hizo zingine, ni lazima kwanza utumie fidia zinazopatikana kwa mujibu wa IDEA (yaani, lalamishi la mchakato yakinifu, mkutano wa kusuluhisha, na taratibu zisizobagua za mchakato yakinifu) kabla ya kuenda moja kwa moja mahakamani.

**Ada za Wakili -** 34 CFR §300.517 Kwenye hatua au taratibu yoyote ya kisheria inayoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ukishinda, mahakama, kwa uamuzi wake pekee, inaweza kukututuza ada za wakili zenye mantiki kama sehemu ya kulipia gharama zako. Kwenye hatua au taratibu yoyote inayoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, mahakama, kwa uamuzi wake pekee, inaweza kutuza ada za mawakili zenye mantiki kama sehemu ya gharama zilizohimiliwa na wilaya ya shule au wakala ya elimu ya jimbo yenye mamlaka, itakayolipwa na wakili wako ikiwa wakili huyo: (a) aliwasilisha lalamishi au kesi ya mahakama ambayo mahakama inaona haina uzito, au haina msingi; au (b) aliendelea kuchukua hatua za kisheria baada ya kuwa wazi kuwa hatua hiyo ya kisheria imekuwa haina uzito, au haina msingi; au kwenye hatua au taratibu yoyote ya kisheria inayoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, mahakama, kwa uamuzi wake pekee, inaweza kutuza ada za mawakili zenye mantiki kama sehemu ya gharama zilizohimiliwa na wilaya ya shule au wakala ya elimu ya jimbo yenye mamlaka, ikiwa ombi lako la kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu, kama vile kunyanyasa, kusababisha ukawiaji usiokuwa lazima, au kuongeza gharama ya hatua au taratibu ya kisheria bila kuhitajika. Mahakama zinatuza ada za mawakili zenye mantiki kama ifuatavyo: (1) Ni lazima ada zitegemee kiasi cha ada cha jumla kwenye jamii ambapo hatua au kesi iliibuka na aina na ubora wa huduma zilizofikishwa. Hakuna kiongezo wala kizidishi kinachoweza kutumiwa ili kung'amua ada zilizotuzwa; (2) Ada zinaweza zisituzwe na gharama husika zinaweza zisifidiwe kwenye hatua au taratibu yoyote ya kisheria kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kwa huduma zilizotekelezwa baada ya chaguo la kusuluhisha la kimaandishi kutumwa kwako ikiwa: (a)Chaguo linapewa ndani ya muda uliobainishwa na Sheria ya 68 ya Sheria za Shirikisho za Taratibu ya Umma au, kuhusiana na kesi ya mchakato yakinifu, kwenye wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya kesi kuanza; (b) chaguo halikubaliwi ndani ya siku 10 za kalenda, na (c) Mahakama au ALJ inang'amua kuwa fidia uliyoipata mwishowe si nzuri kwako kuliko chaguo la kusuluhisha. Licha ya vizuizi hivi, tuzo ya ada za mawakili na gharama husika inaweza kupewa wewe ukishinda kesi na ikiwa ulikuwa na haki ya kulikataa chaguo la kusuluhisha; (3) Ada zinaweza zisituzwe kuhusiana na mkutano wowote wa Timu ya IEP isipokuwa ikiwa mkutano unafanywa kwa mujibu wa matokeo ya hati ya kimahakama au taratibu ya usimamizi; (4)Ada pia zinaweza zisituzwe kwenye upatanishi kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Upatanishi**. Mkutano wa kusuluhisha, kama ulivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Mkutano wa kusuluhisha**, hauchukuliwi kuwa mkutano ulioandaliwa kutokana na matokeo ya kesi ya usimamizi au hatua ya kimahakama, na pia hauchukuliwi kama kesi ya usimamizi au hatua ya mahakama kwa malengo ya matakwa ya ada hizi za mawakili. Mahakama inapunguza, kama ilivyo mwafaka, kiasi cha ada za mawakala zinazotuzwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwa mahakama inang'amua kuwa: (1) Wewe, au wakili wako, wakati wa mwendeleo wa hatua au taratibu ya kisheria, uliufanya uamuzi wa mwisho wa simtofahamu ukawie bila mantiki; (2) Kiasi cha ada za mawakili ambazo kivingine zinaidhinishwa zituzwe zinaikithiri bila mantiki bei kwa kila jisaa kwenye jamii kwa huduma sawia zinazotolewa na mawakili wenye uhodari, sifa, na uzoefu sawia kimantiki; (3)Muda uliotumiwa na huduma za kisheria zilizofikishwa zilikuwa nyingi mno tunapozingatia asili ya hatua au taratibu ya kisheria; au (4)Wakili anayekuwaskilisha hakuipatia wilaya ya shule maelezo mwafaka kwenye notisi la ombi la mchakato yakinifu kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Lalamishi la Mchakato Yakinifu**. Hata hivyo, mahakama huenda isipunguze ada ikiwa mahakama inaamua kuwa jimbo au wilaya ya shule

imeufanya uamuzi wa mwisho wa hatua au taratibu ya kisheria ukawie bila mantiki au kulikuwa na ukiukaji kwa mujibu wa matakwa ya vidhibiti vya kitaratibu vya Sehemu B ya IDEA.

**Taratibu za Kuwarekebisha Tabia Watoto wenye Ulemavu**

**Amri ya Wafanyakazi Shuleni -** 34 CFR §300.530 Wafanyakazi shuleni wanaweza kuzingatia hali yoyote ya kipekee kulingana na kesi binafsi, wanapoamua kama badiliko la mandhari ya shule, linalofanywa kulingana na mahitaji yafuatayo yanayohusu tabia, ni mwaka kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya shule ya tabia ya mwanafunzi. Kwa kiwango ambacho pia wanachukua hatua kama hizi kwa watoto wasiokuwa na ulemavu, wafanyakazi wa wa shule wanaweza, kwa muda usiozidi **siku 10 za shule** kwa mfululizo, kumuondoa mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya tabia ya mwanafunzi kutoka kwenye shule yake ya sasa hadi kwenye mazingira mbadala ya elimu, mazingira mengine, au kutoruhusiwa shuleni kwa muda. Wafanyakazi pia wanaweza kutekeleza uondoaji wa ziada wa mtoto kwa muda usiozidi **siku 10 za shule** kwa mfululizo kwenye mwaka huo huo wa shule kwa ajili ya matukio tofauti ya ukosefu adabu, maadamu uondoaji huo uwe haujumuishi badiliko la mandhari ya elimu (tazama **Badiliko la Mandhari ya Elimu Kwa Sababu ya Kuondolewa kwa ajili ya Ukosefu Tabia** ili kupata ufafanuzi, hapo chini). Pindi mtoto mwenye ulemavu anapoondolewa kutoka kwenye shule yake ya sasa kwa jumla ya siku 10 za shule kwenye mwaka sawia wa shule, ni lazima wilaya ya shule, wakati wa siku zozote zinazofuata baada ya kuondolewa kwenye mwaka huo wa shule, ifikishe huduma kwa kiwango kinachohitajika kwa mujibu wa kichwa kidogo, **Huduma**. Ikiwa tabia iliyokiuka kanuni ya tabia ya mwanafunzi haikutokana na udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto (tazama **Uamuzi wa Udhihirishaji**, hapo chini) na badiliko la mandhari ya elimu kwa ajili ya tabia utazidi **siku 10 za shule** kwa mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutekeleza taratibu za urekebishaji tabia kwa mtoto huyo mwenye ulemavu kwa njia sawia na kwa muda sawia kama vile ingekuwa kwa watoto wasiokuwa na ulemavu, isipokuwa ni lazima shule zifikishe huduma kwa mtoto huyo kama ilivyofafanuliwa hapo chini kwenye **Huduma**. Timu ya IEP ya mtoto inaamua mazingira mbadala ya elimu ya mpito kwa huduma kama hizi.

**Huduma -** Huduma ambazo ni lazima apatiwe mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kwenye shule yake ya sasa zinaweza kupewa kwenye mazingira mbadala ya elimu ya mpito. Wilaya ya shule ni lazima impatie huduma mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kwenye shule yake ya sasa tu kwa **siku 10 za shule au chache zaidi** kwenye mwaka huo wa shule, ikiwa inampatia huduma mtoto asiyekuwa na ulemavu ambaye pia ameondolewa. Michigan hailazimu huduma zipewe wanafunzi wasiokuwa na ulemavu ambao wameondolewa kwa ajili ya sababu za ukosefu adabu. Ni lazima mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kutoka kwenye shule yake ya sasa kwa **zaidi ya siku 10 za shule**: (1) Aendelee kupokea huduma za elimu, ili kumwezesha mtoto aendelee kushiriki kwenye mtaala wa elimu wa jumla, ingawa itakuwa kwenye mazingira mengine, na kuchukua hatua ili kukidhi shabaha zilizobainishwa kwenye IEP ya mtoto; **na** (2) Apokee, kama ni mwafaka, tathmini ya kishughuli ya tabia (FBA), na mabadiliko na huduma za kurekebisha tabia, ambazo zimeundwa ili kuushughulikia ukiukaji tabia ili usiweze kutokea tena. Baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kutoka kwenye shule yake ya sasa kwa **siku 10 za shule** kwenye mwaka sawia wa shule, na ikiwa uondoaji wa sasa ni kwa **siku 10 za shule** kwa mfululizo au chache zaidi **na** ikiwa uondoaji si badiliko la mandhari ya elimu (tazama ufafanuzi hapo chini), basi wafanyakazi wa shule, kwa kushauriana na angalau mmojawapo kati ya walimu hao, wanaamua kiwango ambacho huduma zinahitajika ili kumwezesha mtoto aendelee kushiriki kwenye mtaala wa elimu wa jumla, ingawa ni kwenye mazingira mengine, na kuchukua hatua ili kutimiza shabaha zilizobainishwa kwenye IEP ya mtoto. Ikiwa uondoaji ni badiliko la mandhari ya elimu (tazama ufafanuzi hapo chini), Timu ya IEP ya mtoto huyo inaamua huduma mwafaka ili kumwezesha mtoto aendelee kushiriki kwenye mtaala wa elimu wa jumla, ingawa ni kwenye mazingira mwngine, na kuchukua hatua ili kukidhi shabaha zilizobainishwa kwenye IEP ya mtoto huyo.

**Uamuzi wa udhihirishaji** - Ndani ya **siku 10 za shule** baada ya uamuzi wowote wa badiliko la mandhari ya elimu la mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ukiukaji kanuni ya tabia ya mwanafunzi, (isipokuwa kwa uondoaji ambao ni wa **siku 10 za shule** kwa mfululizo au chache zaidi na sio badiliko la mandhari ya elimu), wilaya ya shule, mzazi, na wanachama husika wa Timu ya IEP (kama ilivyoamuliwa na mzazi na wilaya ya shule) ni lazima wahakiki maelezo yote husika kwenye faili ya mwanafunzi, ikiwemo IEP ya mtoto, mazingatio yoyote ya mwalimu, na maelezo yoyote husika yanayotolewa na wazazi ili kuamua: (1) Ikiwa tabia inayohusika ilisababishwa na, au ilikuwa na uhusiano mkubwa au wa moja kwa moja na, ulemavu wa mtoto; au (2) Ikiwa tabia inayohusika ilitokana moja kwa moja na kushindwa kwa wilaya ya shule kutekeleza IEP ya mtoto. Ikiwa wilaya ya shule, mzazi, na wanachama husika wa Timu ya IEP ya mtoto wanaamua kuwa yoyote kati ya masharti hayo mawili imetimizwa, ni lazima tabia hiyo iamuliwe kuwa ni udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto huyo. Ikiwa wilaya ya shule, mzazi, na wanachama husika wa Timu ya IEP ya mtoto wanaamua kuwa tabia inayohusika ilitokana na kushindwa kwa wilaya ya shule kutekeleza IEP, basi ni lazima wilaya ya shule ichukue hatua papo hapo ili kufidia upungufu huo. Ikiwa wilaya ya shule, mzazi, na wanachama husika wa Timu ya IEP wanaamua kuwa tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, ni lazima Timu ya IEP: (1) Itekeleze FBA, isipokuwa ikiwa wilaya ya shule ilitekeleza FBA kabla ya tabia iliyosababisha badiliko la mandhari ya elimu lililotokea, itekeleze mpango wa kurekebisha tabia (BIP) wa mtoto huyo; au (2) Ikiwa BIP tayari imeundwa, itathmini BIP, na irekebishe, kama inavyohitajika, ili kuishughulikia tabia hiyo. Isipokuwa kama ilivyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa kidogo, **Hali maalum**, ni lazima wilaya ya shule imrudishe mtoto kwenye mandhari ya elimu ambapo mtoto aliondolewa, isipokuwa ikiwa mzazi na wilaya ya shule wanakubaliana na badiliko la mandhari ya elimu kama sehemu ya marekebisho ya BIP.

**Hali Maalum - Mamlaka ya Waajiriwa Shuleni –** Kama tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto au la, waajiriwa shuleni wanaweza kumuondoa mwanafunzi na kumpeleka kwenye mandhari mbadala ya elimu ya kimpito (yanayoamuliwa na Timu ya IEP ya mtoto huyo) kwa hadi siku 45 za shule, ikiwa mtoto: (1) Anabeba silaha shuleni au ameweka silaha shuleni, ndani ya mipaka ya shule, au kwenye hafla ya shule iliyo chini ya mamlaka ya MDE au wilaya ya shule; (2) Kwa kujua, anazo au anatumia dawa haramu, au anauza au anajaribu kuuza madawa yasiyoruhusiwa anapokuwa shuleni, ndani ya mipaka ya shule, au kwenye hafla ya shule iliyoko chini ya mamlaka ya MDE au wilaya ya shule; au (3) Amesababisha jeraha kubwa mwilini mwa mtu mwingine alipokuwa shuleni, ndani ya mipaka ya shule, au alipokuwa kwenye hafla ya shule iliyo chini ya mamlaka ya MDE au wilaya ya shule.

**Ufafanuzi -** *Madawa yasiyoruhusiwa* inamaanisha dawa za kulevya au kitu kingine kinachotambuliwa kwa mujibu wa vifungu vya I, II, III, IV, au V ndani ya kifungu cha 202(c) cha Sheria ya Dawa za Kulevya (21 U.S.C. 812(c)). *Dawa haramu* inamaanisha dawa inayodhibitiwa; lakini haijumuishi dawa inayodhibitiwa ambayo inabebwa au kutumiwa kwa mujibu wa usimamizi wa mtaalamu wa uangalizi wa afya mwenye leseni au inayomilikiwa au kutumiwa kisheria kwa mujibu wa mamlaka mengine yoyote kwenye Sheria au kwenye matakwa yoyote mengine ya sheria ya Shirikisho. *Jeraha kubwa mwilini* ina maana iliyopewa maneno ''jeraha kubwa mwilini'' kwenye paragrafu ya (3) ya kifungu kidogo cha (h) cha kifungu cha 1365 cha mada ya 18, Kanuni ya Marekani. (Tazama Ufafanuzi wa Shirikisho kwenye mwisho wa hati hii.) *Silaha* ina maana iliyopewa neno ''silaha hatari'' kwenye paragrafu ya (2) ya kifungu kidogo cha (g) cha kifungu cha 930 cha mada ya 18, Kanuni ya Marekani. (Tazama Ufafanuzi wa Shirikisho kwenye mwisho wa hati hii).

**Taarifa -** Kwenye tarehe ambapo inafanya uamuzi wa uondoaji shuleni ambao ni badiliko la mandhari ya elimu ya mtoto huyo kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni ya tabia ya mwanafunzi, ni lazima wilaya ya shule iarifu wazazi kuhusu uamuzi huo, na iwapatie wazazi notisi ya vidhibiti vya kitaratibu.

**Badiliko la Mandhari ya Elimu Kwa Sababu ya Uondoaji kwa ajili ya Urekebishaji Tabia -** 34 CFR §300.536 Kumuondoa mtoto mwenye ulemavu kutoka kwenye mandhari ya sasa ya elimu ya mtoto huyo ni **badiliko la mandhari ya elimu** ikiwa (1) Uondoaji ni kwa zaidi ya siku 10 za shule kwa mfululizo **au** (2) Mtoto ameondolewa shuleni mara kwa mara ambayo inajumuisha ruwaza kwa sababu: (a) Jumla ya mfululizo wa uondoaji ni zaidi ya siku 10 za shule kwenye mwaka wa shule; (b) Tabia ya mtoto huyo inafanana sana na matukio ya awali yaliyosababisha mfululizo wa kuondolewa shuleni; na (c) Kwenye sababu hizi za ziada kama vile urefu wa kila uondoaji, jumla ya kiasi cha muda mtoto ameondolewa shuleni, na kwa kiasi gani uondoaji huo unakaribiana. Kama ruwaza ya uondoaji shuleni inajumuisha badiliko la mandhari ya elimu inaamuliwa kwa msingi wa hali maalum na wilaya ya shule na, ikipingwa, inapitia uhakiki kupitia mchakato yakinifu na taratibu za kimahakama.

**Uamuzi wa Mandhari -** 34 CFR § 300.531 Timu ya IEP ni lazima iamue mandhari mbadala ya elimu ya kimpito ya uondoaji shuleni ambao ni **badiliko la mandhari ya elimu,** na uondoaji shuleni kwa mujibu wa vichwa**, Mamlaka ya ziada** na **Hali maalum**, hapo juu.

**Rufaa -** 34 CFR § 300.532 Mzazi wa mtoto mwenye ulemavu anaweza kuwasilisha ombi la lalamishi la mchakato yakinifu (tazama hapo juu) ili kuwasilisha ombi la kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu ikiwa yeye hakubaliani na: (1) Uamuzi wowote kuhusu mandhari ya elimu unaofanywa kwa mujibu wa matakwa haya ya urekebishaji tabia; au (2) Uamuzi wa udhihirishaji uliofafanuliwa hapo juu. Wilaya ya shule inaweza kuwasilisha ombi la kusikizwa kesi ya mchakato yakinifu (tazama hapo juu) ili kuwasilisha ombi la kesi ya mchakato yakinifu ikiwa inaamini kuwa kudumisha mandhari ya sasa ya elimu ya mtoto huyo kuna uwezekano mkubwa wa kumsababishia jeraha mtoto au kuwasababishia jeraha wengine.

**Mamlaka ya hakimu wa sheria ya usimamizi -** ALJ inayokidhi mahitaji yaliyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa kidogo, Hakimu wa sheria ya usimamizi asiyebagua, ni lazima asikize kesi ya mchakato yakinifu na afanye uamuzi. ALJ inaweza: (1) Kumrudisha mtoto mwenye ulemavu kwenye shule ambapo mtoto huyo aliondolewa ikiwa ALJ inaamua kuwa uondoaji shuleni ulikuwa ni ukiukaji wa mahitaji yaliyofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, Mamlaka ya Waajiriwa Shuleni, au kuwa tabia ya mtoto ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto; au (2) Kuagiza badiliko la mandhari ya elimu la mtoto mwenye ulemavu hadi kwenye mandhari mbadala ya elimu ya kimpito na yaliyo mwafaka kwa siku ambazo si zaidi ya siku 45 za shule ikiwa ALJ inaamua kuwa kudumisha shule ya sasa ya mtoto kuna uwezekano mkubwa sana wa kumsababishia jeraha mtoto au watu wengine. Taratibu hizi za kusikizwa kesi zinaweza kurudiwa, ikiwa wilaya ya shule inaamini kuwa kumrudisha mtoto kwenye shule ya awali kuna uwezekano mkubwa sana wa kumsababishia jeraha mtoto na watu wengine.

Wakati wowote mzazi au wilaya ya shule inapowasilisha lalamishi la mchakato yakinifu ili kuwasilisha ombi la kusikizwa kesi kama hii, ni lazima kesi inayosikizwa ikidhi mahitaji yaliyofafanuliwa kwa mujibu wa vichwa**, Lalamishi la Mchakato Yakinifu, Kesi za Malalamishi ya Mchakato Yakinifu,** isipokuwa kama ifuatavyo: (1) MDE inapanga kesi ya mchakato yakinifu inayosikizwa kwa upesi, ambayo ni lazima isikizwe ndani ya siku **20** za shule

baada ya tarehe ambapo kesi iliwasilishiwa ombi na ni lazima ilete uamuzi ndani ya siku **10** za shule baada ya kusikizwa kesi. (2) Isipokuwa ikiwa wazazi na wilaya ya shule wanakubaliana kimaandishi kutofanya mkutano, au wanakubaliana kutumia upatanishi, mkutano wa kusuluhisha ni lazima ufanyike ndani ya siku **saba** za kalenda baada ya kupokea notisi ya lalamishi la mchakato yakinifu. Ni lazima kesi iendelee isipokuwa ikiwa imesuluhishwa kwa kuridhika kwa wahusika wote wawili ndani ya siku **15** za kalenda baada ya kupokea lalamishi la mchakato yakinifu. Uamuzi unaofanywa kwenye kesi ya mchakato yakinifu inayofanywa kwa upesi ni wa mwisho, isipokuwa kuwa mhusika yoyote anayehusishwa kwenye kesi hiyo (wewe au wilaya ya shule) anaweza kuleta hatua ya umma, kama inavyofafanuliwa kwenye kichwa "Hatua za Umma, Zikiwemo Kipindi cha Muda cha Kuwasilisha Hatua Hizo."

**Mandhari ya Elimu Wakati wa Rufaa -** 34 CFR §300.533 Pale, kama ilivyofafanuliwa hapo juu, mzazi au wilaya ya shule imewasilisha lalamishi la mchakato yakinifu linalohusu masuala ya urekebishaji tabia, basi ni lazima mtoto (isipokuwa ikiwa mzazi na MDE au wilaya ya shule mnakubaliana kivingine) abakie kwenye mandhari mbadala ya elimu ya kimpito kwa kusubiri uamuzi wa afisa wa kusikiza kezi, au mpaka kuisha kwa kipindi cha muda kilichobainishwa na kilichofafanuliwa kwa mujibu wa kichwa, **Mamlaka ya Waajiriwa Shuleni**, yoyote inayokuja mwanzo.

**Ulinzi kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Husika -** 34 CFR §300.534 Ikiwa mtoto hajaamuliwa kuwa anastahiki elimu maalum na huduma husika na anakiuka kanuni ya tabia ya mtoto, lakini wilaya ya shule ilikuwa inajua (kama inavyoamuliwa hapo chini) kabla ya kutokea tabia iliyoleta hatua ya urekebishaji, kuwa mtoto huyo alikuwa mtoto mwenye ulemavu, basi mtoto huyo anaweza kudai yoyote kati ya vilinzi vilivyofafanuliwa kwenye notisi hii.

**Msingi wa ufahamu wa masuala ya urekebishaji tabia -** Ni lazima wilaya ya shule ichukuliwe kuwa ina ufahamu kuwa mtoto huyo ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa, kabla ya kutokea tabia iliyoleta hatua ya urekebishaji tabia: (1)Mzazi wa mtoto alieleza wasiwasi wake kimaandishi kuwa mtoto huyo anahitaji elimu maalum na huduma husika kwa waajiriwa wasimamizi wa wakala mwafaka ya elimu, au mwalimu wa mtoto huyo; (2) Mzazi aliwasilisha ombi la tathmini linalohusu ustahiki wa elimu maalum na huduma husika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA; au (3) Mwalimu wa mtoto huyo, au mwajiriwa mwingine wa wilaya ya shule alibainisha wasiwasi maalum kuhusu ruwaza ya tabia aliyokuwa nayo mtoto huyo moja kwa moja kwa mkurugenzi wa elimu maalum wa wilaya ya shule au kwa mwajiriwa mwingine wa usimamizi wa wilaya ya shule.

**Kitengwa -** Wilaya ya shule haingechukuliwa kuwa inajua kuhusu mambo haya ikiwa (1) Mzazi wa mtoto huyo hajaruhusu tathmini ya mtoto huyo au amekataa huduma maalum za elimu; au (2) Mtoto huyo ametathminiwa na ameamuliwa kuwa si mtoto mwenye ulemavu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. Ikiwa kabla ya kuchukua hatua za urekebishaji dhidi ya mtoto huyo, wilaya ya shule haijui kuwa mtoto ni mtoto mwenye ulemavu, kama ilivyofafanuliwa hapo juu kwa mujibu wa vichwa vidogo, **Msingi wa ufahamu wa masuala ya urekebishaji tabia** na **Kitengwa**, mtoto anaweza kuchukuliwa hatua za urekebishaji tabia zinazohusishwa kwa watoto wasiokuwa na ulemavu wanaojihusisha na tabia zinazolingana. Hata hivyo, ikiwa ombi limewasilishwa la tathmini ya mtoto wakati wa kipindi cha muda ambapo mtoto anachukuliwa hatua za urekebishaji, ni lazima tathmini itekelezwe kwa njia ya upesi. Mpaka tathmini ikamilike, mtoto anabakia na hali ya elimu iliyoamuliwa na mamlaka za shule, ambayo inaweza kujumuisha kufukuzwa shuleni kwa muda au milele bila huduma za elimu. Ikiwa mtoto anaamuliwa kuwa ni mwanafunzi mwenye ulemavu, kwa kuzingatia maelezo kutoka kwa tathmini iliyotekelezwa na wilaya ya shule, na maelezo yaliyotolewa na wazazi, ni lazima wilaya ya shule ifikishe elimu maalum na huduma husika kulingana na Sehemu B ya IDEA, ikiwemo mahitaji ya urekebishaji tabia yaliyofafanuliwa hapo juu.

**Uelekezaji hadi Watekelezaji Sheria na Mamlaka za Kimahakama na Hatua Zao -** 34 CFR §300.535 Sehemu ya IDEA: (1) Haikatazi wakala kuuripoti kwa mamlaka mwafaka uhalifu unaofanywa na mtoto mwenye ulemavu; au (2) Haizui watekelezaji sheria wa jimbo kutekeleza majukumu yao kuhusiana na kutekeleza amri ya sheria ya jimbo na shirikisho kwenye uhalifu unaofanywa na mtoto mwenye ulemavu.

**Uwasilishaji wa rekodi -** Ikiwa wilaya ya shule inaripoti uhalifu unaofanywa na mtoto mwenye uhalifu, wilaya ya shule: (1) Ni lazima ihakikishe kuwa nakala za rekodi za tabia na elimu maalum ya mtoto huyo inawasilishwa ili izingatiwe na mamlaka ambazo zimepokea ripoti ya uhalifu kutoka kwa wakala; na (2) Inaweza kuwasilisha nakala za rekodi za tabia na elimu maalum za mtoto huyo tu kwa kiwango kinachoruhusiwa na FERPA.

**Mahitaji ya Kubadilishiwa Mandhari ya Elimu Bila Kutushauri ambayo Inafanywa na Wazazi wa Watoto kwenye Shule Binafsi kwa Gharama ya Umma**

34 CFR §300.148 Sehemu B ya IDEA hailazimu shule ilipie gharama ya elimu, ikiwemo elimu maalum na huduma husika, ya mtoto wako mwenye ulemavu kwenye kituo au shule binafsi ikiwa wilaya ya shule ilifanya FAPE ipatikane kwa mtoto wako na wewe ukachagua kumweka mtoto wako kwenye kituo au shule binafsi. Hata hivyo, ni lazima wilaya ya shule ambapo wilaya ya shule iko imjumuishe mtoto wako kwenye watoto ambao mahitaji yao maalum ya elimu yanashughulikiwa kwenye matakwa ya Sehemu B kuhusu watoto waliowekwa na wazazi wao kwenye shule binafsi kwa mujibu wa 34 CFR §§300.131 hadi 300.144. Ikiwa mtoto wako ashawahi kupokea elimu maalum na huduma husika kwa mujibu wa mamlaka ya wilaya ya

shule, na unachagua kumuandikisha mtoto wako kwenye shule binafsi bila idhini au bila kuelekezwa na wilaya ya shule, mahakama au ALJ inaweza kuishurutisha wakala ikufidie gharama ya uandikishaji ikiwa mahakama au ALJ inaamua kuwa wakala haikufanya FAPE ipatikane kwa mtoto wako kwa muda mwafaka kabla ya uandikishaji huo na kuwa uwekaji kwenye shule binafsi ni mwafaka. ALJ au mahakama inaweza kuamua kuwa wewe kumuingiza shuleni ni mwafaka, hata kama mandhari ya elimu hayakidhi viwango vinavyohusisha elimu inayotolewa na MDE na wilaya za shule. Gharama ya fidia iliyofafanuliwa kwenye paragrafu ya hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa: (1) Ikiwa: (a) Kwenye mkutano wa hivi karibuni zaidi wa IEP uliohudhuria kabla ya wewe kumuondoa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukuifahamisha Timu ya IEP kuwa ulikuwa unakataa shule aliyopewa na wilaya ya shule ili kumpatia FAPE mtoto wako, ikiwemo kubainisha wasiwasi na nia yako ya kumuandikisha mtoto wako kwenye shule binafsi kwa gharama ya umma; au (b) Kwa angalau siku kumi rasmi (ikiwemo sikukuu zozote zinazotokea kwenye siku rasmi) kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukutoa notisi ya kimaandishi kwa wilaya ya shule kuhusu maelezo hayo; (2) Ikiwa, kabla ya wewe kumtoa mtoto wako kwenye shule ya serikali, wilaya ya shule ilikupatia notisi ya kimaandishi mapema, kuwa wilaya ya shule ina nia ya kumtathmini mtoto wako (ikiwemo kauli ya lengo la tathmini ambayo ilikuwa mwafaka na yenye mantiki), lakini hukumfikisha mtoto kwenye tathmini; **au** (3) Baada ya uamuzi wa mahakama kuwa matendo yako hayana mantiki. Hata hivyo, gharama ya fidia: (1) Ni lazima ipunguzwe au ikataliwe kwa ajili ya kushindwa kuwasilisha notisi ikiwa: (a) Shule ilikuzuia kutoa notisi; (b) Ilikuwa hukupokea notisi ya wajibu wako wa kuwasilisha notisi iliyofafanuliwa hapo juu; au (c) Kutii masharti ya hapo juu kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha madhara kwenye mwili wa mtoto wako; na (2) Huenda, kwa uamuzi wa mahakama au ALJ, isipunguzwe wala isikataliwe kwa ajili ya wazazi kushindwa kuwasilisha notisi inayohitajika ikiwa: (a) Mzazi hajui kusoma au hawezi kuandika kwa Kiingereza; au (b) Kutii mahitaji ya hapo juu kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha madhara madhubuti ya kisaikolojia kwa mtoto huyo.

**Uhamishi wa Haki za Wazazi kwenye Umri wa Utu Uzima -** 34 CFR §300.520 Wakati mwanafunzi mwenye ulemavu anapofika umri wa utu uzima (umri wa miaka 18 huko Michigan ikiwa mlezi wa kisheria hajawahi kuteuliwa na mahakama), ni lazima wakala ya umma itoe notisi zozote zinazohitajika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kwa mwanafunzi na mzazi na haki zote anazopewa mzazi kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA zitahamishwa kwa mwanafunzi. Haki zote zinazopewa mzazi pia zinahamishwa hadi kwa wanafunzi waliofika umri wa utu uzima na ambao wametiwa kizuizini kwenye kituo cha urekebishaji tabia cha kienyeji, shirikisho, au jimbo cha watoto au watu wazima.

### Ufafanuzi wa Shirikisho

**Jeraha Kubwa Mwilini** - 18 USC 1365(h) (3) Maneno "jeraha kubwa mwilini" yanamaanisha jeraha mwilini linalohusisha – (A) hatari madhubuti ya kufa; (B) maumivu makali mno mwilini; (C) kulemaa dhahiri kwa muda mrefu; au (D) kulemaa au kupoteza kwa muda mrefu shughuli ya akili, kiungo, au sehemu ya mwili; na (4) Maneno "jeraha mwilini" inamaanisha –(A) kukatika, kukwaruzika, kuumia, kuchomeka, au kulemaa; (B) maumivu mwilini; (C) ugonjwa; (D) kulemaa au kupoteza kwa muda mrefu shughuli ya akili, kiungo, au sehemu ya mwili; au (E) jeraha lolote lingine mwilini, bila kujali ni muda mfupi kwa kiasi gani.

**Silaha -** 18 USC 930(g) (2) Maneno "silaha hatari" yanamaanisha silaha, kifaa, zana, nyenzo au, hai au kisicho hai, kinachotumiwa kwenye, au kilicho tayari, kusababisha kifo au jeraha kubwa mwilini, isipokuwa kuwa neno hili halijumuishi kisu kidogo chenye wembe ulio na urefu wa chini ya inchi 2 1/2.